Teknolojia

## Ndege inayokaa saa 24 angani yaanza safari

Uk. 28

Uchumi

## TPA iwe kioo cha ufanisi kwa mashirika ya umma

Uk. 16

Mzee Tai

## Mbunge kugawa bagia, hajamaliza kazi bado

Safu Uk. 5


# Pambazuko

Toleo Namba 177 Jumatatu, Agosti 10-16, 2026


# Safari ya uhuru wa Lissu kuanza

Uk. 6&7



- Leo kesi yake kusikilizwa mfululizo, huku Jumuiya ya Madola ikishinikiza aachwe huru haraka ikiwa ni ukomo wa sharti lao

## Wadau waingiwa hofu uhalali Tume Jinai

Uk. 20



## Tutakwama kujenga uchumi wa kidijiti

Habari Uk. 8&9

## Ripoti ya LHRC kuhusu haki yaibua mazito

Uk. 22

## Rwanda yavuruga wauza pombe kali

Habari Uk. 22

Tafakuri ya Bagonza

## Enyi CCM tujifunze kuweka akiba ya maneno

Safu Uk. 10

## Tahariri

# Tulinde tunu za Tanzania kwa wivu mkubwa

MIONGONI mwa mambo makubwa ambayo Pambazuko limeapa kuyapigania, ni kulinda na kuhimiza Tanzania yenye amani, maendeleo makubwa yanayogusa kila mwananchi.

Kinachofanywa na gazeti hili kuhakikisha haya tunayopigania yanalindwa kwa wivu mkubwa ni kuendelea kuhimiza Watanzania kuthamini na kujivunia kuwepo kwa utulivu, uzalendo na utu.

Hizi ni tunu halisi zinazoliunganisha taifa letu kuwa wamoja zaidi. Ni urithi tulioupokea kutoka kwa waasisi wa taifa hili, na ambao kwa muda mrefu umetuwezesha kuishi kwa mshikamano licha ya tofauti zetu za kikabila, kidini na kisiasa.

Hata hivyo, katika miaka ya hivi karibuni, kumekuwepo na dalili na mahali pengine kuthibitika kutetereka kwa tunu hizo.

Hili linathibitishwa na kuongezeka kwa kauli za chuki, kuporomoka kwa uvumilivu, na hisia za kuaminiana kati ya wananchi na viongozi wao na hata baadhi ya taasisi, zimeanza kuyumba.

Hali hii siyo ya kupuuzwa, kwani ni hatari kwa ustawi wa taifa na mustakabali wa vizazi vijavyo. Taifa lisilojenga juu ya misingi ya amani na utu haliwezi kusonga mbele kwa utulivu na maendeleo endelevu.

Ni muhimu kutambua kuwa amani hujengwa na kulelewa, na kwamba ni matokeo ya juhudi za makusudi, ambazo zinahitaji uongozi wenye busara, wananchi wenye nidhamu, na mifumo inayotenda haki.

Sisi Pambazuko tunawaomba viongozi wetu katika ngazi zote kutambua uzito wa dhamana waliyopewa. Wafanye kazi kwa bidii na uadilifu, watende haki bila upendeleo, na wajiepushe na vitendo vya ubadhirifu, matumizi mabaya ya madaraka na mienendo mingine isiyofaa.

Wananchi wanapoona wazi kwamba kuna maeneo ambapo uongozi na utumishi wa umma umegeuka kuwa eneo la kuchuma isivyokuwa halali au hata kuwa fimbo ya kuwachapa, imani yao hupungua na mshikamano wa kitaifa kudhoofika.

Viongozi wanapaswa kuwa mfano wa kuigwa. Wanapaswa kuonyesha kwa vitendo kwamba madaraka ni kwa ajili ya kuhudumia, siyo kutawala kwa nguvu. Uongozi unaosikiliza, unaojali na unaowajibika, ndio msingi wa kurejesha imani ya wananchi na kuimarisha umoja wa kitaifa.

Katika kutekeleza wajibu wao, wananchi wanapaswa kuendelea kuheshimu sheria, kufanya kazi kwa bidii, kutumia maarifa kujiletea maendeleo na kuchangia kwa dhati katika ustawi wa taifa.

Uzalendo wa kweli hauishii kwenye maneno; unaonekana katika vitendo; kulinda mali za umma, kulipa kodi kwa uaminifu, kuheshimu haki za wengine na kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo ya jamii.

Tanzania ni yetu sote, na hatuna nchi ya ziada ya kukimbilia endapo tutaivuruga sisi wenyewe - kwa njia zozote zile.

Lakini kila mmoja akiamua kulinda tunu zetu kwa uaminifu mkubwa na wivu usiopimika, hakika leo yetu itakuwa yenye manufaa makubwa, huku tukijihakikishia kesho yenye amani, haki na maendeleo kwa kila Mtanzania.

# Uzinduzi mwendokasi




*Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan akikata utepe kuashiria kufungua rasmi huduma ya mabasi ya mwendokasi katika Barabara ya Kilwa, Chang'ombe, Sokoine na Kawawa kwenye hafla iliyofanyika Mtoni kwa Aziz Ally, jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. Picha na Ikulu.*

## Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **"HABARI"** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: info@pambazuko.or.tz** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Unaweza kusoma gazeti hili kupitia tovuti ya **www.rifaly.com**


## TIMU YA PAMBAZUKO

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Mhariri Mkuu** | : | Simon **MKINA** | (simon@pambazuko.or.tz) |
| **Mhariri Mtendaji** | : | Peter **NYANJE** | 0784 211 716 |
| **Mwandishi Mkuu** | : | Elizabeth **HOMBO** | 0712 792 216 |
| **Mwandishi Mwandamizi** | : | Andrew **MSECHU** | 0769 415 815 |
| **Mkuu wa DTP** | : | Yassin **LUPATU** | 0782 009 971 |
| **Mkuu wa Utawala** | : | Tryruckia **MFINANGA** | 0744 768 263 |

*Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A – nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435; Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz*

# Dunia: Hapa na Pale

## Kunguru wazua hofu Kenya

KUNDI la kunguru weusi  wanaojulikana kwa kuharibu mazingira na kuangamiza ndege wa asili, limezua hofu baada ya kuonekana kwa mara ya kwanza jijini Nairobi.

Hii imewalazimu wataalamu wa uhifadhi wa mazingira kuingia kazini kutafuta chanzo cha ujio wao.

Ndege hao wavamizi ambao asili yao ni India, walionekana awali katika Soko la Burma na taarifa kuwafikia wataalamu wa uhifadhi, ambao walifika na kuthibitisha hofu hiyo bada ya kueleza kuwa ni ndege wanaotoka Mombasa, zaidi ya kilomita 400 kutoka pwani ya jiji hilo.



## "Jesus I Love You" yamponza

DEREVA mmoja nchini Uingereza, Simeon Chandra, amejikuta matatani baada ya kampuni ya bima kumtaka afute neno "Jesus I Love You" kwenye gari yake, kwa maelezo kwamba haitaendelea kumhudumia iwapo hatafuta neno hilo.

Kampuni hiyo ya bima ya GoSkippy, ilieleza kuwa dereva huyo amekiuka mkataba wao, kwa kuwa wakati akilisajili gari hilo neno hilo halikuwepo, hivyo haitomtambua kutokana na maboresho hayo aliyoyafanya baadaye, kwa kuweka neno hilo ubavuni mwa gari.

Dereva huyo hakuwa na namna zaidi ya kukubaliana na maelekezo ya mteja wake, ili aweze kuendelea kupata haki yake ya bima, wakati mwenyewe akiendelea kuwasiliana na wanasheria wake hasa kuhusu uhuru na haki yake ya kueleza imani yake hadharani.

## Kuzaliwa siyo kigezo cha" Umarekani"

HAKI ya kuzaliwa Marekani sasa haitamhakikishia mtoto kupata uraia moja kwa moja wa taifa hilo kubwa kiuchumi na kijeshi duniani.

Hii ni baada ya Rais Donald Trump kutia saini amri mbili mpya, zinazolenga kupunguza haki ya uraia wa kuzaliwa nchini humo.

Hatua hiyo inakuja wiki chache baada ya Mahakama Kuu kukataa jaribio lake la awali la kufuta haki hiyo, amri inayopanua orodha ya raia wa kigeni ambao watoto wao wanaozaliwa Marekani, kuwa hawatapata uraia wa moja kwa moja wa Marekani.

Amri ya pili inapiga marufuku kile kinachoitwa "utalii wa kujifungua" ambapo wanawake wajawazito husafiri kwenda Marekani kujifungua ili watoto wao wapate uraia wa Marekani kwa kuzaliwa. Trump amesema' "Hatua hii ilipaswa kuchukuliwa miaka mingi iliyopita."

## Meta yaingia matatani

KAMPUNI ya Meta inayoendesha mitandao ya kijamii ya Facebook na Instagram, imeingia matatani baada ya jaji wa Marekani katika Jimbo la New Mexico kuiamuru kulipa dola milioni 567 (pauni milioni 421).

Hukumu hiyo ni baada ya kushindwa kuionya jamii kuhusu hatari ambazo majukwaa yake yanawahusu watoto, ikiwa ni hukumu kubwa zaidi dhidi ya kampuni hiyo kuhusiana na usalama wa watoto mtandaoni.

Katika hukumu hiyo iliyotolewa mwishoni mwa wiki, Jaji Bryan Biedscheid alisema kuwa kampuni ni "kero kwa umma" inayofanana na uchafuzi wa hewa, na kwamba lazima iweke fedha hizo kwenye mfuko unaolenga kupunguza madhara ya baadaye.

Hukumu hiyo inaongezeka juu ya faini ya dola milioni 375 ambayo Meta ilikuwa tayari imeamriwa kulipa katika kesi hiyo, na kufanya jumla ya malipo kuwa dola milioni 942.

Na Mzee TAI

# Mbunge kugawa bagia, hajamaliza kazi bado

NIMEMUONA kijana wangu Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, Patrick Mwalunenge, akigawa visheti, bagia, soda, machungwa na mihogo ya kuchemshwa kwa wananchi wake.

Furaha iliyolipuka – wananchi wengi waliokuwepo ilikuwa kubwa kiasi kwamba - kwa dakika chache, ilionekana kama vile barabara zote zimewekwa lami, maji yamefika kila nyumba na vijana wote wamepata ajira.

Wananchi wakionekana kushangilia, waligombea soda, wengine wakashika miwa, na wenye bahati wakaondoka na mihogo ya kuchemshwa.

Hakika matumbo kwa waliobahatika kupata mlo, yakatulia na ndimi zikapata utamu wake na hilo likafanya haki-tumbo kutendewa inavyostahili.

Hakika siyo vibaya mbunge kuwakaribia watu wake au kuwapa walau kitafunwa, lakini tatizo huanza pale bagia zinapotaka kupewa hadhi ya daraja, kisheti kuitwa zahanati na soda kuwasilishwa kama sera ya maendeleo.

Wabunge wengi huamini kuwa wanapogawa vitafunwa kwa wananchi, basi hoja zao nazo zimetafunwa na kumalizika. Hawa waheshimiwa hujenga hoja kwamba maendeleo huletwa na serikali, siyo wao.

Wanasahau kwamba miwa huisha utamu, chungwa hubaki maganda na mihogo hushibisha kwa saa chache, lakini ukosefu wa maji, ajira, dawa hospitalini, masoko ya wakulima na barabara nzuri hubaki palepale, ukiwasubiri viongozi wenye mipango na uthubutu.

Ieleweke kuwa kazi ya mbunge siyo kuendesha kantini ya kisiasa, bali mbunge hutumwa bungeni kutunga sheria, kuisimamia serikali, kuhoji matumizi ya fedha za umma na kupigania bajeti inayogusa maisha ya wananchi.

Anatakiwa kujua shida za jimbo lake, kuzipanga kwa vipaumbele na kuzifuatilia kwa uthabiti hadi zipatiwe majibu kutoka serikalini. Hapo ndipo uwakilishi unapogeuka kuwa maendeleo, badala ya onyesho la dakika chache mbele ya kamera.

Wananchi nao wanapaswa kujifunza kutofautisha kati ya zawadi na haki. Kisheti ni zawadi; maji safi ni haki. Bagia ni kitafunwa; shule bora ni haki. Soda ni burudani; huduma nzuri za afya ni haki. Chungwa linaweza kufurahisha ulimi leo, lakini mradi wa umwagiliaji unaweza kuilisha nchi kwa miaka mingi.

Kwa hiyo, kila mbunge anapofika na kapu la vitafunwa, wananchi wavitafune kwa furaha - washibe, lakini wasisahau kufungua daftari la madai, na kuanza kuhoji ahadi za uchaguzi zimefikia wapi?

Wahoji endapo bajeti ya jimbo imeongezeka kwa kiasi gani? Vijana wameandaliwa mikopo na maeneo ya biashara? Barabara, shule na vituo vya afya vinaendeleaje? Majibu ya maswali hayo ndiyo kipimo cha uongozi.

Mbunge mwenye weledi hafurahii kofi pekee; anatafuta matokeo. Hataki wananchi wawe watazamaji wa ukarimu wake, bali washiriki kwa kupanga maendeleo yao.

Mwakilishi wa wananchi anatakiwa kutumia ubunifu kuvutia uwekezaji, kufungua masoko, kuhamasisha miradi na kuhakikisha serikali inawajibika. Akitoa mihogo, ni vizuri; lakini aeleze pia mkakati wa kuongeza thamani ya mazao ya wakulima.

Mwalunenge na wabunge wengine wakumbuke kuwa wananchi hawakuwachagua kuwa wagawaji wa utamu, bali watetezi wa kesho yao. Vitafunwa vinaweza kujenga ukaribu, lakini haviwezi kuchukua nafasi ya uwajibikaji na mwisho wa muhula, wapigakura hawapaswi kuhesabu visheti walivyokula; wanapaswa kuhesabu miradi iliyokamilika, huduma zilizoboreshwa na fursa zilizopatikana.

Mheshimiwa mimi Mzee Tai, sina shida ukigawa vitafunwa na hata chakula kabisa cha mchana ama jioni, lakini wakati unafanya ukarimu huu hakikisha unachochea kupatikana kwa maendeleo yenye mizizi.

Tambua kuwa tumbo linaweza kushiba leo; historia itakuuliza uliwajengea nini wananchi wako kwa kesho. Maendeleo hayawekwi kwenye sahani; hujengwa kwa mipango, uwajibikaji, ubunifu na matokeo yanayopimika katika maisha ya wananchi wote.

Habari Kuu

# Safari ya uhuru wa Lissu kuanza



Na Mwandishi WETU

KUNA dalili kwamba serikali inajipanga kuachana na mashitaka dhidi ya Tundu Lissu, Mwenyekiti wa Chama cha Demorasia na Maendeleo (Chadema), ambaye anakabiliwa na kesi ya uhaini.

Akiwa korokoroni kwa siku 106 hadi sasa, kesi yake imepangwa kuanza kusikilizwa katika Mahakama Kuu ya Tanzania, masjala ndogo ya Dar es Salaam, kuanzia leo Agosti 10 hadi Septemba 7, 2026.

Taarifa ambazo zimefika kwa Pambazuko zinaeleza kuwa upo uwezekano mkubwa kwa kiongozi huyo wa upinzani kuwa huru, kwa serikali kueleza kwamba "haina nia ya kuendelea na kesi."

Kumekuwepo na shinikizo kubwa kutoka kwa taasisi, mashirika na hata baadhi ya nchi kuhimiza kuachiwa kwa Lissu, ikielezwa kuwa mashitaka yake yamejikita kwenye masuala ya kisiasa kuliko uzito wa mashitaka yenyewe.

Hata hivyo, serikali mara zote imekuwa "ikijiweka pembeni" madai ya kushinikiza Lissu aendelee kushitakiwa kwa maelezo kwamba haiwezi kuingilia uhuru wa mahakama.

**Mtego wa Madola**

Pamoja na kuwa ni ratiba iliyopangwa tangu awali, lakini usikilizwaji wa kesi hiyo wakati huu inaonekana kama hatua muhimu kwa serikali kujaribu kujinasua katika mtego uliowekwa na Kundi la Mawaziri wa Jumuiya ya Madola la Demokrasia na Haki za Binadamu (CMAG).

Mtego uliowekwa na CMAG ni kuwepo kwa masharti baada ya kumtuma mjumbe wake, Lazarus Chakwera, Rais (mstaafu) wa Malawi, kuja kufuatilia hatma ya vurugu za wakati na baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka jana, ni kuachiwa kwa kiongozi huyo wa upinzani ambaye yuko rumande kwa takribani mwaka mmoja sasa.

Kesi hiyo inaanza kusikilizwa katika siku ya mwisho iliyowekwa na kundi hilo la mawaziri wa CMAG ambayo ni leo, Agosti 10, kupitia uamuzi wake kikao chao cha 73 kilichofanyika Julai 10, 2026 kwa dharura.

Mawaziri hao walitoa tamko la kuhitimisha, baada ya kujadili hali ya kisiasa na haki za binadamu hapa nchini Tanzania.

Kesi hiyo inatarajiwa kuvuta hisia na usikivu mkubwa wa umma nchini, huku jopo la mawakili wake likithibitisha kuwa limejipanga kikamilifu kuendelea na mapambano ya kisheria Mahakama Kuu.

Kesi hiyo imepangwa kusikilizwa kwa siku 27 mfululizo na wengi wanadhani kuwa muda huo umepangwa mahsusi ili kuisogeza mbele kesi hiyo kwa haraka.

Katika ujumbe wake alioutoa kwa umma kupitia kwa mmoja wa mawakili wake, Paul Kisabo, waliomtembelea gerezani Ukonga, Dar es Salaam - Agosti 6, 2026, Lissu aliomba Watanzania wamuombee.

Inaendelea Uk. 7

# Safari ya uhuru...

Inatoka Uk. 6

Katika ujumbe wao uliotolewa Julai 10, 2026, kundi la mawaziri hao wa CMAG katika kikao chao cha 73 walieleza kuwa Tanzania iko kwenye "rada zao" ikifuatiliwa kuhusu masuala ya haki za binadamu na utawala bora.

Miongoni mwa mambo ambayo CMAG iliainisha kutoridhishwa nayo ni kile walichokieleza kuwa ni kuzidi kuzuiliwa kwa shughuli za kisiasa nchi nzima, kubinywa kwa uhuru wa asasi za kiraia, mitandao ya kijamii na vyombo vya habari kwa ujumla.

CMAG pia ilieleza kusikitishwa kwake na uamuzi wa kuendelea kushikiliwa kwa kiongozi mkuu wa upinzani, Tundu Lissu, na wanasiasa wengine walioko mahabusu au magerezani.

### Masharti

Katika kikao hicho cha 73, CMAG ilitoa mwongozo ikitaka Serikali ya Tanzania iondoe vizuizi vya uhuru wa kukusanyika, kujieleza, asasi za kiraia na vyombo vya habari, iandae jukwaa la mashauriano ya vyama vya siasa.

CMAG pia ilitoa maelekezo ya muda maalumu wenye ukomo,  yenye ukomo wa muda ambapo walitaka kutatuliwa kwa suala la kushikiliwa kwa Lissu kupitia njia za kisiasa au kisheria ndani ya siku 30, na kuwaachia wengine wote wanaoshikiliwa kwa kutumia haki zao kwa amani.

Pia ilielekeza kurejeshwa kwa upatikanaji kamili wa mitandao ya kijamii na kuacha vitisho dhidi ya vyombo vya habari na watetezi wa uhuru wa kujieleza ndani ya siku 60 na kuitishwa jukwaa shirikishi lenye kuaminika la vyama vya siasa (likiongozwa na mwezeshaji huru) ndani ya siku 90 ili kujadili mabadiliko ya mfumo wa uchaguzi, ushindani wa kisiasa, wafungwa, na uwajibikaji.

Mawaziri hao pia walielekeza kuanza uchunguzi huru wa makosa ya jinai uliopendekezwa na Tume ya Uchunguzi, pamoja na fidia kwa wahanga, mambo ambayo huenda yakaingia katika ajenda yao muhimu kwenye vikao vijavyo vya Septemba na Novemba 2026 ambavyo vitatoa hitimisho kuhusu mwelekeo wa Tanzania katika jumuiya hiyo.



### Uzito wa kesi ya Lissu

Lissu alikamatwa Aprili 9, 2025 na Jeshi la Polisi akiwa Mbinga, Ruvuma, muda mfupi baada ya kumaliza mkutano na baadaye akafunguliwa kesi ya uhaini.

Baadaye Aprili 15, 2026, Dkt. Chakwera alikutana na Lissu akiwa gerezani Ukonga jijini Dar es Salaam na katika kikao hicho, Lissu alitoa masharti na mapendekezo saba yanayolenga kulinda demokrasia na kuondoa kesi za uhaini dhidi yake ili kupisha maridhiano.

Huenda mwito huo wa Jumuiya ya Madola ndiyo majibu ya kikao hicho cha Lissu na Chakwera.

Serikali ilimshtaki Lissu kwa uhaini na kuchapisha taarifa za uongo mtandaoni, kwa madai kuwa kampeni ya "No Reforms, No Election" ilichochea uasi wa umma.

Katika kesi yake inayoendelea - ambayo imeahirishwa mara nyingi, Lissu aliomba kujiwakilisha mwenyewe baada ya jopo lake la mawakili kudai kuwa walinyimwa fursa ya kuwasiliana naye kwa faragha na hivyo kujiondoa kwenye kesi hiyo.

Hata hivyo, serikali imekuwa ikisisitiza kuwa kesi inayomkabili Lissu haijachochewa kisiasa na mahakama ipo huru katika kuisikiliza.

■ Habari

# Tutakwama kujenga uchumi wa kidijiti



Waziri wa Fedha Balozi Khamis Mussa Omar

**Na Mwandishi WETU**

KUPITIA bajeti ya 2026/27 Serikali ya Tanzania imeonesha dhamira yake ya kujenga uchumi wa kidijiti.

Ili kutekeleza azma hiyo serikali ilipeleka bungeni mabadiliko ya Sheria ya Fedha, ambayo tayari yamepitishwa.

Mabadiliko hayo, pamoja na mambo mengine, yanaweka msingi wa nchi, kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuanza kukusanya ushuru na kodi kupitia biashara zinazofanywa mitandaoni na wazawa pamoja na wageni.

Kupitia mabadilijko hayo, serikali imepiga hatua kubwa ya kisheria kwa lengo la kujumuisha uchumi wa kidijiti katika mfumo wa kodi.

Sheria hii inalenga kupanua wigo wa kodi kwa kutotoza ushuru wa bidhaa (excise duty) na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa huduma za kidijiti zinazotolewa na kampuni yasiyo na makazi nchini (non-residents).

Hata hivyo, uchunguzi wa kina wa vifungu vya sheria hii unabaini pengo kubwa kati ya madhumuni ya kisheria na maandalizi ya miundombinu ya utekelezaji.

Tofauti na nchi kama Kenya, Afrika Kusini, na mataifa ya Umoja wa Ulaya (EU), ambazo zilianza kwa kujenga mifumo thabiti na rahisi ya usajili wa kidijitali, ukusanyaji, na mifumo ya kiutawala kabla ya kuanza kubana utekelezaji , Tanzania imeweka wajibu wa kisheria bila kubainisha mifumo halisi ya kiutendaji jinsi kodi hizo zitakavyokusanywa na kusimamiwa.

Kutokamilika kwa maandalizi ya utekelezaji wa sheria hiyo, kumethibitishwa na mmoja wa wakurugenzi wa TRA ambaye Pambazuko liliwasiliana naye kutaka kujua jinsi mamlaka hiyo ilivyoanza utekelezaji wa sheria hiyo.

"Utaratibu unafanyiwa kazi," alijibu mkurugenzi huyo kwa ufupi.

Pambazuko lilitaka ufafanuzi wa utaratibu uliowekwa na TRA jinsi wafanyabiashara, hasa wale wasio na makazi Tanzania, watakavyohusishwa katika ulipaji kodi na jinsi watakavyosajiliwa kuwa walipa kodi bila ya kuwa na makazi nchini.

Pambazuko pia lilimwomba mkurugenzi huyo aeleze utaratibu uliowekwa na TRA kuwatambua Watanzania wanaofanya biashara kupitia mitandao ya kijamii ili nao waingizwe kwenye mfumo wa VAT kama mawakala wa kukusanya kodi hiyo.

Pia, Pambazuko liliuliza iwapo kuna mfumo wowote mahsusi ulioanzishwa au kuwekwa kwa ajili ya wafanyabiashara hawa kujiandikisha iwapo watataka kufanya hivyo.

Lakini jibu hilo fupi linaonyesha kuwa hakuna maandalizi yaliyofanyika kwa ajili ya utekelezaji wa sheria hiyo muhimu inayolenga kupeleka Tanzania kwenye uchumi wa kidijiti.

**Mabadiliko ya sheria**

Sheria ya Fedha ya Mwaka 2026 imefanya mabadiliko katika sheria kuu tatu ili kudhibiti uchumi wa kidijitali.

Inaendelea Uk. 9

# Tutakwama kujenga

Inatoka Uk. 8

Kwanza, imefanya mabadiliko kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa kwa Huduma za Kidijitali (sura 147).

Chini ya mabadiliko hayo yaliyo katika kifungu cha 8, Kifungu cha 126 cha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa kimerekebishwa ili kuanzisha utaratibu wa kutoza ushuru wa bidhaa kwenye huduma za kidijitali zinazotolewa na kampuni za kigeni kwa wateja walio nchini Tanzania kupitia mtandao wa intaneti au njia nyingine za kielektroniki.

Chini ya mabadiliko hayo ya sheria, watoaji wa huduma hizi wanatakiwa kujisajili, kuwasilisha ritani za kodi na kulipa ushuru.

Pili, mabadiliko yamefanyika katika Sheria ya VAT kwa Masoko ya Kidijitali (sura 148) ambapo kifungu cha 94 (kinachorekebisha Kifungu cha 51 cha Sheria ya VAT) kinamfanya mwendeshaji wa soko la kidijitali (digital marketplace operator au intermediary) kutambulika kama mtoa huduma rasmi kwa madhumuni ya VAT.

Hii inajumuisha majukwaa kama vile tovuti, programu za simu (apps), na milango ya intaneti (internet portals).

Tatu, kuna mabadiliko ya sheria ya Urasimishaji wa Malipo ya Kielektroniki (sura 185).

Mabadiliko katika kifungu cha 6 cha Sheria ya Miamala ya Kielektroniki sasa yanampa waziri husika  mamlaka ya kuagiza malipo fulani kufanyika kwa njia ya kielektroniki, ikijumuisha sharti la kuwa na uthibitisho wa malipo ya kielektroniki wakati wa kuhamisha umiliki wa ardhi, majengo na vyombo vya moto.

**Madhumuni ya mabadiliko, walengwa**

Mabadiliko ya Sheria ya Fedha ya Mwaka 2026 yanalenga kampuni kubwa za kimataifa zinazotoa huduma bila kuwa na ofisi (physical presence) nchini.

Mifano ya huduma na makampuni yanayolengwa ni pamoja na; huduma za utiririshaji (Streaming Services) kama vile zinazotolewa na kampuni za Netflix, Spotify, Disney+, Amazon Prime Video.




Pia mabadiliko hayo yamelenga kampuni zinazotoa huduma za software (Cloud & SaaS) kama vile Amazon Web Services (AWS), Microsoft Azure, Google Cloud, Microsoft 365, Adobe Creative Cloud, Zoom na Salesforce.

Mabadiliko pia yanalenga maduka ya programu za simu (App Stores) kama vile Apple App Store na Google Play Store.

Mabadiliko hayo pia yanahusu matangazo ya mtandaoni yanayotolewa na kampuni kama Google Ads, Meta (Facebook & Instagram Ads) na LinkedIn Ads.

Aidha, kampuni zinazotoa huduma za akili unde (AI) kama vile OpenAI (ChatGPT Plus/API), Anthropic Claude API, Google Gemini, nayo pia yanalengwa na mabadiliko ya sheria hiyo.

**Kasoro nyingine**

Sheria ya Fedha ya 2026 inaunda mfumo wa kujitathmini mwenyewe (self-assessment regime), bila kuweka taratibu au miundombinu ya kiutendaji wa suala hilo iliyokamilika.

Pia, sheria inatamka kuwa usajili, uwasilishaji wa ritani, na ulipaji wa ushuru utafanyika "kulingana na kanuni zitakazotungwa na waziri". Lakini, mwezi mmoja baada ya sheria hiyo kuanza kutumia, bado haijatangazwa kama kanuni hizo zimetungwa.

Inaendelea Uk. 14

Tafakuri ya Bagonza



Na Dkt. Benson BAGONZA



# Enyi CCM tujifunze kuweka akiba ya maneno

SIKU chache kabla na baada ya vikao vya Chama Cha Mapinduzi (CCM) huko Zanzibar – Julai 28-29, 2026), wana CCM tumekuwa na maneno yanayovuka heshima kubwa tuliyo nayo kuliongoza taifa.

Naomba niwakumbushe kwamba ni hatari kujifanya kuhisi kuzorota kwa uhusiano kati ya rais, makamu, Rais wa Zanzibar na waziri mkuu. Hata inapotokea kuhisi; tusiwe wepesi kushtaki au kuleta hoja ya kujua zaidi ya wao wanavyojuana. Ukijiweka mbele halafu wao wakapatana? Utaomba hifadhi Malawi?

Yanayozungumzwa sasa kuhusu makamu wa rais hayawezi kuwa yametokana na inayoitwa hotuba kwa wanaharakati. Siyo mwanzo na siyo kilele.

Katika mihemko ya mjadala unaogusa hizo nguzo nne, usitumie neno ambalo utakosa pa kuweka uso wako baada ya kinachoitwa mgogoro kuisha.

Urais na umakamu havitenganishwi kihivyo. Ukimkashifu makamu, na rais amekashifiwa na kinyume chake. Msividhalilishe hivyo viti viwili katika kimoja kwa namna ambayo itavifanya visitamike tena. Kuna maisha baada ya mjadala huu.

Mfumo wa mgombea mwenza ulikuja baada ya mjadala mkali ulioongozwa na Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere katikati ya changamoto kali za Muungano. Chokochoko za sasa ndani ya chama zirudi nyuma na kujielimisha hekima iliyotumika.

Maswali niliyouliza kuhusu hotuba ya Katiba mpya yamejibiwa. Wanaozuia Katiba mpya ni makundi mawili; kwanza, ni wana CCM wanaomchukia mwana CCM anayewapa watu matumaini ya Katiba mpya. Pili, ni wapinzani wanaokimbilia Katiba mpya kabla ya maridhiano ya KWELI. Upo kundi gani?

Rais na makamu ni mali ya Watanzania wote. Wakiishaapishwa siyo mali ya CCM pekee. CCM tusile na kipofu tukamgusa mkono.

Makamu wa rais ni mwanasiasa. Ni sauti ya rais na mwakilishi wake ndani na nje. Ni msaidizi wa rais, siyo msaidiwa wa rais. Ni rais tu, mwenye haki isiyohojiwa, kutilia shaka anavyosaidiwa. Wengine tupunguze viherehere vyetu vinavyokuza tatizo.

Kwao wote wawili, watambue kuwa wanaongoza nchi iliyojeruhiwa. Nchi inahitaji kutunzwa kuliko nchi kuwatunza wao. Siasa iko mikononi mwa vyombo na wana harakati. Propoganda zinajenga wapinzani na mabeberu kuliko zinavyowabomoa. Mungu awape ujasiri wa kukubali ukweli kuwa kuna kitu hakiko sawa.

Agenda ya Gen Z isiishie kuiundia wizara. Vijana ni agenda ngumu na tete. Tumewaona Amecea wakijadili. Mashirika yote ya dunia yameweka mikakati kwa vijana. Tushtuke tunapomuondoa “Millenial” na kumleta “Baby Boomer.” Kwa Gen Z tuache itikadi wala mikopo. Tunawatumia, hatuwasililizi. Tutaumia!

***Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.***



Na Dkt. Hellen Kijo BISIMBA

Kona ya Dkt. Bisimba

# Hakuna ugaidi au kuna viashiria? Tumwamini nani?

KUNA kauli ambazo zimetolewa na viongozi wawili katika wizara moja, tena ndani ya kipindi kifupi.

Waziri wa Mambo ya Ndani, Patrobas Katambi alisema hakuna ugaidi nchini, bali kunaweza kuwa na viashiria vya matendo ya kigaidi.

Waziri Katambi alisema haya wakati akijaribu kufafanua suala la kukamatwa watu na akajaribu kuonyesha jinsi ambavyo hakuna mtu aliye juu ya sheria na tunaongozwa na Katiba, Sheria ya Kanuni ya Adhabu na hata Sheria ya Ugaidi.

Katika maelezo yake, akaweka msisitizo kuwa Tanzania hakuna ugaidi.

Lakini kabla yake tuliisikia kauli ya Msemaji wa Jeshi la Polisi, David Misime, akisema hadi wakati huo jeshi hilo lilikuwa limewakamata watu 130 kwa tuhuma zinazohusiana na ugaidi.

Katika maelezo yake Misime alieleza wapo waliokamatwa na vilipuzi na wako waliosikika wakila njama ya kuua viongozi wa serikali, kuwanyang'anya polisi silaha, kuharibu miundombinu ya umeme na kukata miti ili kuwazuia polisi wasifike kwa urahisi kutoa msaada.

Na kwa kuonyesha kuwa Jeshi la Polisi linajua jambo linalolifanya katika suala hili la ugaidi tayari limeshawafikisha watu 36 mahakamani kwa tuhuma za ugaidi. Hadi hatua hiyo, hapo suala la ugaidi hauwezi kulichukulia kama propaganda tu, kwani limeshachukuliwa hatua kisheria.

Hapa mwananchi aamini kauli ipi? Waliamini Jeshi la Polisi ambalo limeshachukua hatua za kukabiliana na ugaidi au tumwamini waziri ambaye anasisitiza kuwa hakuna ugaidi!

Kama tukimwamini waziri, ina maana kuwa Jeshi la Polisi limewakamata watu kwa tuhuma ambazo hazipo!

Lakini Jeshi la Polisi limeshawafikisha watu mahakamani kwa tuhuma za ugaidi. Siamini kuwa chombo hiki mahiri katika ulinzi wa sheria kinaweza kuchukua hatua kali kama hii kwa kuzingatia tu kuwa kuna viashiria.

Umma unahitaji ufafanuzi utakaoondoa mkanganyiko hasa kwa kuwa ugaidi ni jambo hatari sana.

Hili ni tishio kubwa, siyo hapa nchini tu bali hata kwa wageni ambao wanaitembelea nchi yetu kama watalii, wanafunzi, watafiti, wafanyabiashara, viongozi au wawekezaji.

Suala la ugaidi ni zito kiusalama nchini na duniani, ambalo hapa nchini lina sheria mahsusi. Katika kuongelea masuala ya kiusalama katika taifa tahadhari kubwa inahitajika katika utoaji wa taarifa.

Kauli zinazotoka kwa viongozi zinatakiwa ziwe zinazoweza kujenga imani, kutoa mwelekeo mmoja na kuhakikisha wananchi wanaelewa hali halisi bila kupatwa na hofu wala kupotoswa.

Unahitajika uwepo wa uwazi unaofaa na mawasiliano yanayowiana kwani hilo nalo ni sehemu ya usalama.

Tukiangalia pia upande mwingine kwa hawa wageni nchini, wawekezaji na hata wadau wa maendeleo uthabiti wa taarifa zilizo rasmi ni jambo la muhimu na la msingi sana.

Unapotoka ujumbe unaoonekana kutofautiana au usioonekana bayana kimaana na kimantiki yanaweza kuzuka maswali kwao ni ipi hali halisi ya usalama katika nchi.

Taswira ya nchi hujengwa siyo kwa hali ya usalama ilivyo, bali pia kwa namna mamlaka zinavyowasiliana kuhusu hali hiyo.

Kwa hali kama hizi mamlaka inapaswa kuelezea kwa uwazi tofauti zilizopo kati ya 'viashiria vya ugaidi' 'tuhuma za ugaidi' na 'uwepo wa ugaidi.'

Umuhimu wa ufafanuzi huu ni kuwawezesha wananchi kuelewa kinachoendelea na waweze kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama kwa msingi wa taarifa sahihi na zinazoeleweka.

Ukiangalia hizo ni dhana tofauti kabisa zinazopaswa kuangaliwa kwa vile hayo ni mambo tofauti kabisa kisheria na hata kiusalama.

Katika masuala nyeti kiasi hiki, kauli zinazolingana na zinazofafanua hali halisi siyo jambo la hiari, ni sehemu ya kujenga imani ya umma kwa muktadha wa kulinda maslahi ya taifa.

***Mwandishi wa safu hii ya kila wiki, ni mwanaharakati wa demokrasia, haki za binadamu na mwanazuoni wa falsafa ya sheria. Anapatikana kwa namba 0713 337240.***

Habari

# Rwanda yavuruga wauza pombe kali




Na Mwandishi WETU

SERIKALI ya Rwanda imeibua sintofahamu miongoni mwa wazalishaji, wasambazaji na wauzaji wa pombe kali katika nchi za Afrika Mashariki.

Nchi hiyo imepiga marufuku aina 52 za vinywaji vinavyozalishwa katika nchi sita na kuingizwa nchini humo.

Marufuku hiyo inatokana na kile ambacho kimeelezwa kuwa pombe hizo kutokidhi viwango na kwamba ni hatari kwa afya za watumiaji.

Katika marufuku hiyo, kwa Tanzania inahusisha aina 14 za vinywaji vikali vikiwemo maarufu vya Konyagi, K-Vant na Tzee, ambavyo vimetawala katika masoko ya ndani ya nchi hiyo.

Katika taarifa yake ya Jumatano Agosti 5, 2026, Mamlaka ya Chakula na Dawa Rwanda (Rwanda FDA) ilitangaza kupiga marufuku uagizaji, usambazaji, na uuzaji vinywaji hivyo 52 na kufunga viwanda vinane vya ndani vinavyozalisha pombe kali.

Mamlaka hiyo ya Rwanda ilieleza kuwa hatua hiyo ilitokana na kutokea kwa vifo vya watu zaidi ya 50 vilivyoripotiwa kati ya Januari na Juni 2026 na wengine zaidi ya 100 kupoteza uwezo wa kuona baada ya kunywa pombe zisizo salama.

**Wazalishaji watikiswa**

Akizungumzia suala hilo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Shirikisho la Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Deogratius Massawe alisema hatua hiyo ya Serikali ya Rwanda siyo ya kuchukuliwa kwa wepesi kwa kuwa zuio hilo halihusishi bidhaa za Tanzania pekee, bali pia za ndani ya nchi hiyo, nchi nyingine za Afrika Mashariki za nje ya Afrika.

Massawe alilieleza Pambazuko kuwa katika ufuatiliaji wa awali, ameona agizo hilo likitolewa kama mkakati wa ndani wa taifa hilo kuzuia unywaji pombe uliopitiliza, baada ya Rais Paul Kagame kuhutubia moja ya mkutano wa vijana ambapo alieleza namna ambavyo nguvu kazi imekuwa ikitatizwa na unywaji pombe holela wa vijana, hasa pombe kali.

“Kwa Rawanda, wale wako tofauti kidogo na hizi nchi zetu nyingine. Inaonekana kama hilo tayari lilikuwa agizo kutoka kwa Rais Kagame na huenda muda siyo mrefu ikipitishwa sheria rasmi...”

“Lakini kwa muda huu bado tunaendelea na juhudi za kujua uhalisia wa agizo hilo na kuangalia iwapo kweli zuio hilo linaheshimu makubaliano ya kibiashara baina ya nchi zetu...”

“Mara zote tunapokutana tunanadi soko la nchi zetu za Afrika Mashariki, na hapa ninaona ubaya unaoweza kujitokeza ni kwa nchi nyingine ambazo Rwanda inapeleka bidhaa zake, nazo zinaweza kuchukua tahadhari kali dhidi ya baadhi ya bidhaa zao. Lakini hadi sasa bado tunatoa nafasi kwao ili waeleze kwa kina sababu za hatua hiyo, huenda zikawa zenye mashiko, tutajua namna ya kwenda nao,” alisema.

Alieleza kuwa katika juhudi za awali, TPSF imefanya mawasiliano na Balozi wa Rwanda nchini Tanzania ambaye tayari amekubali kukutana nao siku chache zijazo kuzungumzia suala hilo, ambapo watataka kujua kwa undani sababu za hatua hiyo.

Amesema kwa sasa maswali ambayo wengi wanaendelea kujiuliza mambo kadhaa iwapo hatua ya kuzuia na kutaka mzigo wote uliokuwepo wakati wa agizo hilo urejeshwe kwa wenyewe ni sahihi.

Inaendelea Uk. 13

# Rwanda yavuruga

Inatoka Uk. 12

**Wazalishaji washituka**

Pambazuko lilifanikiwa kuwafikia baadhi ya wazalishaji wa ndani, ambapo mmoja wa watendaji ndani ya Kampuni ya Tanzania Breweries Limited (TBL) ambayo kinywaji kilichoko chini yao cha Konyagi kimeguswa, alieleza kuwa kwa sasa hawawezi kusema lolote kwa kuwa ndiyo wamelipokea na ni jambo ambalo hawakulitarajia.

"Kwa upande wetu, tunaendelea kufanya mawasiliano na tunaliona liko katika upeo wa kiserikali zaidi..."

"Sisi tunaendelea kufuatilia kwa mamlaka zinazohusika na tutatoa taarifa yetu rasmi tutakapojiridhisha kuhusu athari na hasara halisi tutakayokuwa tumeipata kupitia agizo hilo," alieleza huku akikataa jina lake kutajwa gazetini.

Serengeti Breweries Limited (SBL) ambayo baadhi ya vinywaji vyake navyo vimeguswa, msemaji wa kampuni hiyo, Timoth Msoffe alilieleza Pambazuko kuwa wamepata taarifa hiyo na wanaifanyia kazi hasa kwa ajili ya kuangalia athari wanazoweza kuzipata kama wazalishaji na hata kwa wasambazaji wao.

"Kwa sasa athari za moja kwa moja zinakwenda kwa wasambazaji tunaofanya nao biashara, ambao ndio wanaochukua mzigo kwetu na kupeleka nje hasa huko Rwanda..."

"Tumepata taarifa hizo na tunaendelea kufanya juhudi za kuwasiliana na ubalozi wa Rwanda nchini na taasisi zinazosimamia biashara kati ya Tanzania na nchi za nje ili kujua hatua tunazoweza kuchukua kwa sasa," alisema.

**Ubalozi wakaa kimya**

Mmoja wa maofisa wa ubalozi wa Rwanda nchini aliyefikiwa na Pambazuko alisema hawezi kuzungumza lolote kwa kuwa yeye siyo msemaji wa ubalozi, hivyo balozi atakuwa katika nafasi nzuri ya kuzungumzia suala hilo baada ya kumalizika kwa mapumziko ya mwishoni mwa wiki.

**Wizara yavuta pumzi**

Mkurugenzi Mawasiliano katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mindi Kassiga alisema kwa sasa suala hilo linahusika zaidi na mamlaka za Rwanda na jumuiya za wafanyabiashara kwa kuwa limetolewa na Mamlaka ya Chakula na Dawa ya Rwanda (Rwanda FDA) na inahusiana na suala la ubora.

Alisema kwa hatua hii, wanaohusika moja kwa moja na suala hilo ni mamlaka ya viwango nchini, ubalozi wa Rwanda na mamlaka nyingine zinazohusiana moja kwa moja na wazalishaji wa ndani wanaouza bidhaa zao huko.

Balozi huyo alisema kabla ya kufika katika hatua ya wizara kuingilia, kuna mamlaka nyingi ambazo zinatakiwa kulishughulikia katika hatua za awali na iwapo zikikwama ndipo Wizara itakapochukua hatua, hasa kwa kuzingatia matokeo ya ukaguzi na uthibitisho wa ubora kama ambavyo nchi husika inahitaji kulingana na viwango vyake.

**Taarifa ya Rwanda FDA**

Mamlaka ya Chakula na Dawa ya Rwanda, ikitumia sheria na nchini humo na kwa maslahi ya afya ya umma, iliwaeleza waagizaji, wasambazaji, wauzaji rejareja na umma kwa ujumla kwamba uingizaji wa vinywaji vyenye pombe vilivyoorodheshwa katika kiambatisho umesimamishwa kwa muda na kuwa agizo hilo limeanza kutumika mara moja.

FDA ya Rwanda iliwaagiza waagizaji wa bidhaa hizo kuanza mara moja kurudisha bidhaa hizo, kuwaagiza wasambazaji wa bidhaa za kigeni kurejesha bidhaa zilizoorodheshwa kutoka kwa wateja wao.

Kurudisha hisa za sasa na bidhaa zilizorejeshwa kwa waagizaji na waagizaji kuwasilisha ripoti za kurejeshwa kwa bidhaa ndani ya siku tatu za kazi tangu kuchapishwa kwa tangazo hilo, yaani kufikia leo, Jumatatu Agosti 10, 2026.

Pia FDA ya Rwanda iliwaagiza wasambazaji na wauzaji rejareja wote wa bidhaa zilizoorodheshwa kuacha mara moja usambazaji na uuzaji wao, na kuwarejeshea waagizaji wao kiasi kilichobaki mara moja na watumiaji wa vileo vilivyoorodheshwa kuacha mara moja matumizi yao na marufuku ya matangazo yote na nyenzo za utangazaji wa vileo zilizoorodheshwa lazima ziondolewe mara moja kutoka popote zinapoonyeshwa.

Kati ya bidhaa zilizopigwa marufuku nyingi zinatokea nchini India yenye bidhaa 20 ikifuatiwa na Tanzania (bidhaa 14), Uganda (11), Kenya (5), Burundi (1) na Poland (1).

■ Habari

# Tutakwama kujenga

Inatoka Uk. 9

Aidha, sheria yenyewe haianzishi mfumo au tovuti rasmi ya mtandaoni itakayotumiwa na kampuni za kigeni kujisajili, njia za malipo ya fedha za kigeni au sarafu zitakazotumika kulipia ushuru huo pamoja na fomu na tarehe za mwisho za kuwasilisha ritani hizo.

Haya ni mambo muhimu ambayo yanahitajika ili kuufanya mfumo huo ufanye kazi vizuri lakini bado hayapo hadi hivi sasa.

Kwa upande mwingine, sheria hiyo ya fedha iliyobadilishwa haijatoa mamlaka au maelekezo ya kiutendaji kwa TRA kuhusu namna ya kuwachukulia hatua watoa huduma wa kigeni watakaokaidi sheria hiyo.

**Wengine wanafanyaje?**

Umoja wa Ulaya (EU) ulipoanzisha sheria za VAT kwa huduma za kielektroniki, uliunda mfumo ujulikanao kama Mini One Stop Shop (MOSS) na baadaye One Stop Shop (OSS) ambao unarahisisha ukusanyaji wa kodi hiyo.



Mfumo huu uliruhusu kampuni zisizo na makazi katika umoja huo kujisajili katika nchi moja mwanachama na kuwasilisha VAT kwa njia rahisi ya mtandaoni kabla ya sheria kuanza kubana kwa kikamilifu.

Kwa upande wake, Afrika Kusini iliporoboresha sheria zake za VAT kwenye huduma za kidijiti, Mamlaka ya Mapato ya Afrika Kusini (SARS) iliweka mfumo maalum wa mtandaoni uliorahisishwa (simplified VAT registration portal for non-residents) na kutoa miongozo ya wazi ya kiutawala miaka kadhaa kabla ya kupanua wigo wa usajili kwa kampuni za kigeni.

Kwa jirani zetu Kenya, kupitia Mamlaka ya Mapato (KRA) ilipoanzisha kodi ya huduma za kidijitali (Digital Service Tax - DST) na VAT on Digital Supplies, iliweka lango maalum la mtandaoni (iTax portal section for non-residents) linaloruhusu wageni kusajili kwa haraka bila kuweka masharti magumu ya kuwa na muwakilishi wa ndani (local tax agent), pamoja na kutoa miongozo ya kiutendaji sambamba na uanzishwaji wa sheria.

Tanzania, kwa upande mwingine, imeweka matakwa ya kisheria kwenye Sheria ya Fedha bila kuwa tayari kwa mfumo ulioboreshwa wa TRA wa mtandaoni ulioundwa maalum kwa ajili ya kampuni zisizo na makazi nchini.

Wachumi wameliambia Pambazuko kuwa hatua ya Tanzania kutunga sheria ya kutoza kodi uchumi wa kidijiti ni hatua sahihi na muhimu kiuchumi ili kulinda wigo wa kodi wa taifa.

Hata hivyo, wanashauri kuwa ili kutatua pengo kati ya sheria na utekelezaji ni muhimu kwa TRA na Wizara ya Fedha kutoanza tu kwa kutangaza sheria, bali kwa kukamilisha mambo kadhaa ikiwamo kutunga kanuni zitakazoeleza kwa kina taratibu za usajili, ulipaji, na uwasilishaji wa ritani kwa njia ya mtandaoni.

Pia taasisi hizo zianzishe mfumo uliorahisishwa wa usajili kwa njia ya mtandao na kuanzisha mashauriano na kampuni kubwa za teknolojia (Meta, Google, Netflix, Apple) ili kuhakikisha kuwa zinatekeleza sheria hiyo kwa ufanisi.

# WFP yaonya madhara makubwa El Niño

Na Mwandishi WETU

ENEO la Afrika Mashariki, limetakiwa kujiandaa kwa madhara makubwa yatakayotokana na hali ya hewa ya El Nino inayotarajiwa kuikumba dunia baadaye mwaka huu.

Shirika la Chakula Duniani (WFP), katika ripoti yake ya hivi karibuni imeonya kuwa takribani watu milioni 49 duniani kote wapo katika hatari ya kukabiliwa na upungufu mkubwa wa chakula kutokana na El Nino.

WFP inasema hali hiyo inatarajiwa kutokea hadi kufikia mwishoni mwa mwaka huu.

Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika yametajwa kama maeneo ambayo nayo yataathirika zaidi na hali hiyo.

Zaidi ya watu milioni 18 katika maeneo hayo mawili wanatarajiwa kukabiliwa na upungufu mkubwa wa chakula ikiwa ni ongezeko la asilimia 26 ikilinganishwa na viwango vya sasa.

Lakini kwa nchi za Afrika Mashariki athari zinaenda mbali zaidi ya suala la upungufu wa chakula na kutikisa uchumi wa nchi hizo.

Kwa mujibu wa taarifa zilizopo, hali hiyo ya El Nino itaathiri kwa kiasi kikubwa uzalishaji katika sekta ya kilimo.

Wachumi wanaonya kuwa kilimo ni moja ya sekta ambazo zinaajiri watu wengi katika eneo hilo, hivyo kuna uwezekano wa mapato ya watu binafsi na yale ya serikali kuyumba kwa kiasi kikubwa na hivyo kuathiri uchumi.

Nchi nyingi katika eneo hilo hutegemea pia kuongeza mapato yake ya mauzo ya nje kutokana na kilimo inaelezwa kuwa athari za El Nino zinaweza kusababisha kushuka kwa mapato hayo na hivyo kuathiri uwezo wa serikali hizo kuwahudumia wananchi wake.

Inaelezwa pia kuwa viwanda vya kusindika mazao, ambavyo kwa kiasi kikubwa vinategemea malighafi kutoka kwenye kilimo, navyo vitaathirika kwa kukosa malighafi za kutosha.

Hivyo, WFP inaonya kuwa changamoto za tabianchi zinaweza kuwa hatari kubwa ya kiuchumi zinazoweza kupunguza kasi ya ukuaji, kuongeza mfumuko wa bei na kuweka shinikizo kwenye bajeti za serikali.



El Niño inatarajiwa kufikia kilele chake kati ya Septemba na Desemba mwaka huu, lakini athari zake kiuchumi zinaweza kuendelea hadi mwaka 2027 kutokana na kuvurugika kwa misimu ya mvua na kilimo.

Tofauti na ukame au mafuriko ya kawaida, El Niño inaweza kusababisha mifumo tofauti kabisa ya hali ya hewa katika maeneo yanayokaribiana.

Baadhi ya maeneo yanaweza kupata mvua nyingi zinazosababisha uharibifu wa mazao, barabara na miundombinu ya kuhifadhi chakula, huku maeneo mengine yakikumbwa na vipindi virefu vya ukame vinavyopunguza uzalishaji wa kilimo na tija ya mifugo.

**Athari hasi**

WFP inabainisha kuwa kupungua kwa uzalishaji wa mazao bila shaka kutapunguza upatikanaji wa chakula, kuongeza shinikizo la kupanda kwa bei na kuongeza gharama za maisha wakati serikali zikijitahidi kudhibiti mfumuko wa bei ndani ya viwango vinavyolengwa.

Wakati Benki Kuu zinaweza kukabiliwa na shinikizo la kuongeza ukali wa hali ya kifedha, lakini uwezo wa wananchi kununua unaweza kupungua, huku bidhaa zitokanazo na kilimo sokoni zikipanda bei kutokana na ongezeko la gharama za uzalishaji.

Makala



# TPA iwe kioo cha ufanisi kwa mashirika ya umma

**Na Elizabeth HOMBO**

UWEKEZAJI na maboresho yanayoendelea katika Bandari ya Dar es Salaam na bandari nyingine nchini tayari "mavuno" yake yameanza kuonekana.

Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) – kwa miaka mitatu mfululizo, imekuwa kinara miongoni mwa taasisi za umma kwa kutoa gawio kubwa serikalini, ikiwa ni ushahidi kwamba uongozi wenye dira, uwekezaji sahihi, weledi na uwajibikaji vinaweza kubadilisha taasisi ya umma.

Mwaka 2026, TPA imetoa gawio la Shilingi bilioni 205.5, kutoka 181.54/- mwaka 2025 na 153.917/- mwaka 2024.

Kwa wastani, gawio limekuwa likiongezeka kwa takribani Shilingi bilioni 26 kila mwaka.

Mwenendo huu unaonyesha kuwa TPA haitimizi tu malengo yake ya mapato, bali pia huanzia pale ilipoishia mwaka uliotangulia na kuweka viwango vipya vya utendaji.

Inaendelea Uk. 17

# TPA iwe kioo...

Inatoka Uk. 16

Mafanikio hayo yamechangiwa na uwekezaji mkubwa wa Serikali ya Awamu ya Sita, inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, pamoja na ushirikiano na sekta binafsi kupitia DP World na Tanzania East Africa Gateway Terminal Limited.

Maboresho ya miundombinu, usimamizi na huduma yameongeza uwezo wa bandari kuhudumia meli kubwa na mizigo mingi kwa ufanisi zaidi.

Yapo maboresho mengi yaliyofanywa na yanaendelea ikiwamo kuongezwa kwa kina cha magati kadhaa katika Bandari ya Dar es Salaam na bandari zingine ili kuruhusu meli kubwa zaidi kutia nanga.

Katika kipindi cha miaka minne, TPA imeweza kuongeza shehena zinazopokelewa na kusafirishwa nje ya Tanzania kutoka tani milioni 23 mwaka 2023/2024 hadi tani milioni 27 mwaka 2024/2025.

Wakati huohuo, muda wa kuhudumia meli umepungua kutoka siku saba hadi siku tatu. Haya siyo mafanikio kwenye karatasi, ni mabadiliko yanayohisiwa na wafanyabiashara na wasafirishaji, huku malalamiko kuhusu ucheleweshaji yakipungua kwa kiasi kikubwa.

Kuimarika kwa huduma kumevutia zaidi wateja wa ndani na kutoka nchi jirani, zikiwamo Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Zambia, Burundi, Rwanda na Zimbabwe. Hivyo, Bandari ya Dar es Salaam inazidi kuimarisha nafasi yake kuwa lango muhimu la biashara na uchumi wa Afrika.

Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Plasduce Mbossa, amehusisha mafanikio hayo na uwekezaji, miundombinu bora, weledi na kuachana na utendaji wa mazoea.

Kauli hiyo ya mtendaji mkuu wa mamlaka hiyo, inabeba somo muhimu; taasisi ya umma haiwezi kupata matokeo mapya ikiwa itaendelea kufanya kazi kwa mtindo wa zamani.

Gawio la TPA ni zaidi ya takwimu kwenye karatasi, kwani fedha hizo zinaisaidia serikali kujenga barabara, hospitali, vituo vya afya na zahanati, kununua dawa na vifaa tiba, kuboresha huduma za jamii na kupunguza utegemezi wa mikopo ya nje. Kwa hiyo, ufanisi wa TPA una manufaa ya moja kwa moja kwa Watanzania.

Kutokana na mafanikio hayo, mashirika mengine ya umma yanapaswa kuiangalia TPA kama kioo cha kujipima.

Yanahitaji viongozi wanaoelewa dhamana zao, bodi zenye uwezo, watumishi wenye nidhamu, uwekezaji wenye tija, ubunifu, uwazi na malengo yanayopimika. Serikali nayo iendelee kuyawekea mazingira bora na kuyawajibisha.

TPA imeonyesha kuwa shirika la umma linaweza kujiendesha kwa ufanisi, kushindana, kuongeza mapato na kutoa gawio kubwa.

Mfano huu ukiigwa, Tanzania itaimarisha uchumi wake, kupanua huduma kwa wananchi na kupunguza utegemezi wa fedha kutoka nje.

Na mashirika mengi yakifikia viwango vya TPA na hata kuipiku, hapo ndipo mashirika ya umma yatakapokuwa injini halisi za maendeleo ya Tanzania na watu wake.



*Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Plasduce Mbossa*



# Serikali yazengea soko la hewa ukaa

Na Mwandishi WETU

WAKATI dunia ikiweka mkazo kwenye biashara ya hewa ukaa, Tanzania nayo imeamua isiachwe nyuma katika safari hiyo.

Sasa Tanzania imetangaza mipango kadhaa inayolenga kuiwezesha nchi kupata sehemu kubwa zaidi ya mapato kupitia soko la hewa ukaa linalokua kwa kasi duniani.

Kituo cha Kitaifa cha Ufuatiliaji wa Kaboni (NCMC) kimepewa jukumu la kuimarisha mifumo ya usimamizi, kuvutia uwekezaji wa kijani na kuongeza manufaa yatokanayo na rasilimali asilia za nchi.

Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dkt. Richard Muyungi, amesema Tanzania inapaswa kubadilika kutoka kuwa mshiriki wa kawaida katika soko la hewa ya ukaa na kuwa miongoni mwa nchi zinazoongoza kwa kujenga mifumo thabiti inayowezesha utekelezaji wa miradi yenye viwango vya juu vya uadilifu wa kaboni.

Akizungumza wakati wa kikao cha kwanza cha Bodi ya Wakurugenzi ya NCMC kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kilichofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni, Dkt. Muyungi alisema uchumi kupitia hewa ya ukaa ni fursa muhimu kwa Tanzania kuongeza mapato ya taifa huku ikiendelea kuchangia juhudi za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

“Changamoto yetu sasa siyo kushiriki tu katika masoko ya kaboni, bali ni kuyaongoza masoko hayo,” alisisitiza.

Kwa mujibu wa watalaamu wa biashara hiyo, Tanzania, ambayo ina eneo kubwa kijiografia, ina vigezo vyote muhimu kuiwezesha kuikamata biashara hiyo.

Dkt. Muyungi alisema soko la hewa ya ukaa duniani kwa sasa lina thamani ya zaidi ya dola bilioni 107 za Marekani kwa mwaka, huku Afrika ikitarajiwa kuzalisha takribani dola bilioni sita kila mwaka ifikapo mwaka 2030 kupitia soko hilo endapo itatumia kikamilifu fursa zilizopo.

Dkt. Muyungi alisema Tanzania ipo katika nafasi nzuri ya kunufaika na sekta hiyo kutokana na kuwa na rasilimali kubwa za misitu, maeneo oevu, mifumo ya ikolojia ya pwani na baharini, pamoja na fursa zilizopo katika nishati safi na kilimo kinachozingatia mabadiliko ya tabianchi.

Alifichua kuwa hadi sasa Tanzania imesajili miradi 99 ya kaboni, huku zaidi ya mikopo ya kaboni milioni 13.4 ikiwa tayari imetolewa.

Hata hivyo, alionya kuwa nchi bado haijatumia kikamilifu thamani ya kiuchumi inayoweza kupatikana kupitia miradi hiyo.

“Mafanikio haya hayaonyeshi manufaa kamili tunayotarajia kutoka kwenye sekta ya kaboni. Tunahitaji kuhakikisha miradi hii inaingia katika hatua ya utekelezaji na kuanza kuzalisha thamani halisi kwa taifa na jamii,” alisema.

# Kielelezo cha dhamana kuboresha uwazi na uwekezaji

Na Saidina MSANGI

SERIKALI imezindua kielelezo cha viwango vya faida vya dhamana za serikali, hatua inayotarajiwa kuimarisha uwazi wa soko la fedha, kuongeza ufanisi wa maamuzi ya uwekezaji na kuvutia mitaji ya ndani na nje ya nchi.

Kielelezo hicho kilizinduliwa jijini Dar es Salaam wiki iliyopita na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Emmanuel Tutuba, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, Balozi Khamis Mussa Omar.

Akizungumza katika hafla hiyo, Tutuba alisema kupitia kielelezo hicho wawekezaji wataweza kuona na kufuatilia mwenendo wa faida halisi katika soko la upili la dhamana za serikali, jambo litakalowasaidia kufanya maamuzi ya uwekezaji kwa kuzingatia taarifa sahihi na zinazoaminika.

"Kielelezo hicho kitawawezesha wawekezaji wa ndani na wa kimataifa kulinganisha viwango vya faida vya dhamana za serikali na fursa nyingine za uwekezaji ndani ya nchi, pamoja na masoko ya kikanda na kimataifa, hivyo kuongeza uwazi wa soko, kuvutia wawekezaji wa kigeni na kuimarisha ushindani wa soko la fedha nchini," alisema Tutuba.

Aidha, Tutuba alisema Kielelezo hicho pia kitaakisi matarajio ya soko kuhusu ukuaji wa uchumi, mfumuko wa bei na mwelekeo wa sera ya fedha, hivyo kitakuwa nyenzo muhimu kwa Benki Kuu katika kuimarisha utekelezaji wa sera ya fedha inayotegemea viwango vya riba.

"Soko letu limeshuhudia ukuaji mkubwa katika kipindi cha miaka 25, ambapo mwaka 2001, dhamana za Serikali ambazo zilikuwa hazijaiva zilifikia Shilingi bilioni 499, na kuongezeka mpaka kufikia Shillingi trilioni 32.3 hivi sasa," alisema Tutuba.

Pia alibainisha kuwa uthaminishaji wa dhamana za Serikali zinazowasilishwa na benki za biashara kama dhamana ya kupata mikopo kutoka Benki Kuu utafanyika kwa kutumia kielelezo hicho, hatua inayotarajiwa kuongeza usahihi na




uwazi katika shughuli za kifedha.

Aliwashukuru wadau wote wa soko kwa ushiriki wao ambao umeiwezesha serikali kupata fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo kupitia dhamana za Serikali pamoja na kuanza utekelezaji wa Dira ya Taifa ya 2050.

Alisisitiza kuwa kuna umuhimu wa Benki Kuu na Serikali kwa ujumla kuendelea kutoa elimu ya uwekezaji ili kuhakikisha soko linaendelea kukua kwa kasi na kuongeza idadi ya wawekezaji kutoka 32,631 walioko sasa kwani idadi hiyo ni ndogo ikilinganishwa na idadi ya watu nchini.

Awali, akizungumza katika tukio hilo, Kamishna wa Idara ya Usimamizi wa Madeni, Wizara ya Fedha, Japhet Justine, alisema kuwa soko la hisa limeendelea kukua ambapo katika mwaka wa fedha 2025/26, thamani ya miamala iliyofanyika ilikuwa zaidi ya Shilingi trilioni 6.7.

Mkurugenzi Mtendaji wa Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE), Peter Nalitolela, alisema kuwa Kielelezo hicho kitaongeza miamala na ukwasi katika soko la dhamana na kuchochea maendeleo ya aina nyingine za mali zinazouzwa katika soko la hisa.

Habari

# Wadau waingiwa hofu uhalali Tume Jinai


Petrus Tileinge Damaseb

Na Mwandishi WETU

HATUA ya Rais Samia Suluhu Hassan kuzindua Tume ya Uchunguzi wa Makosa ya Jinai yenye jukumu la kuchunguza vurugu zilizotokea wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 29, 2025, imewaibua wadau mbalimbali wakipinga uhalali wake.

Tume hiyo haipingwi tu hapa nyumbani kwani hata huko Namibia, ambako anatoka mmoja wa wajumbe wake, kumeibuka upingaji pia.

Taasisi inayojihusisha na harakati za kisiasa nchini Namibia, Affirmative Repositioning (AR) imepinga uteuzi wa Jaji Mkuu Msaidizi wa Namibia, Petrus Tileinge Damaseb, kushiriki kwenye tume hiyo.

Tume hiyo yenye wajumbe sita; wanne kutoka Tanzania na wengine wawili wakitoka nje ya Tanzania - mmoja kutoka Uganda na mwingine Namibia - ilizinduliwa na Rais Samia, Agosti 7, 2026 Ikulu jijini Dar es Salaam.

Tume hiyo mpya inayoongozwa na Jaji wa Mahakama ya Rufani, Shabani Lila ni sehemu ya utekelezaji wa hatua zilizopendekezwa baada ya kuundwa kwa Tume ya Rais ya Uchunguzi wa Matukio ya Vurugu za Oktoba mwaka jana.

Itakuwa na jukumu la kuchunguza wahusika wa ghasia na ukiukwaji wa sheria na kutoa mapendekezo kuhusu hatua zinazoweza kuchukuliwa.

Kwa mujibu wa adidu za rejea, tume hiyo mpya ina jukumu la kwenda hatua moja mbele ya Tume ya Matukio – iliyoongozwa na Jaji Mkuu (mstaafu) Othman Chande na kuangalia uwepo wa jinai.

Tume hii inapaswa siyo tu kueleza kilichotokea, bali kutafuta nani alihusika na kwa namna gani, ili kuweka msingi wa watu kuwajibishwa kijinai.

Hata hivyo, muda mfupi baada ya tume hiyo kuzinduliwa, AR ilitoa taarifa kwa vyombo vya habari wakipinga uteuzi wa Jaji Damaseb.

Sababu walizotoa kwenye taarifa hiyo ni kwamba hatua hiyo inaweza kuathiri taswira ya uhuru wa Mahakama ya Namibia.

AR imedai kuwa uteuzi huo wa Jaji Damaseb ulitokana na ombi lililowasilishwa na Rais Samia baada ya ziara ya Rais wa Namibia, Netumbo Nandi-Ndaitwah, nchini Tanzania hivi karibuni.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Ofisi ya Mahakama ya Namibia ilithibitisha kuwa ombi hilo lilikuwa la kumteua jaji anayehudumu au aliyestaafu kushiriki katika Tume ya Jinai ya Tanzania.

"AR inahofia ushiriki wa Jaji Damaseb katika tume hiyo kwani unaweza kuathiri uaminifu na hadhi ya Mahakama ya Namibia, kwa sababu majaji wanaohudumu hawapaswi kushiriki katika uchunguzi wa kisiasa wa nchi nyingine…"

"Aidha, ripoti ya tume hiyo anayokwenda kufanya kazi haitarajiwi, kuakisi uchunguzi huru wa matukio yaliyojitokeza wakati na baada ya uchaguzi wa Tanzania wa Oktoba 2025," inasema sehemu ya taarifa hiyo.

Taarifa hiyo iliendelea kudai kuwa vyama tawala vya SWAPO (Namibia) na Chama Cha Mapinduzi (CCM), vinaendeleza ushirikiano wa kisiasa unaotanguliza maslahi ya viongozi kuliko misingi ya haki za binadamu na utawala wa sheria.

Inaendelea Uk. 21

# Wadau waingiwa...

Inatoka Uk. 20

Taarifa hiyo pia ilirejea hali ya viongozi wa upinzani na mazingira ya kisiasa yanayoendelea nchini kama sehemu ya hoja zao za kupinga uteuzi huo.

Mbali na hayo, AR ilitoa mwito kwa Tume ya Utumishi wa Mahakama ya Namibia (JSC) kueleza misingi ya kisheria na kimaadili iliyotumika katika mchakato wa uteuzi huo wa Jaji Damaseb.

Katika hatua nyingine taasisi hiyo ilimtaka Jaji Damaseb kukataa uteuzi huo na kujiondoa katika tume hiyo ili kulinda hadhi ya Mahakama ya Namibia.

"Endapo hatua hiyo haitachukuliwa, AR itatumia njia mbalimbali zikiwamo za kisheria kupinga uteuzi huo na tutaendelea kuunga mkono vijana, wanaharakati na makundi ya kiraia nchini Tanzania katika juhudi za kutafuta haki na uwajibikaji," inasema taarifa hiyo.

Pamoja na wanaharakati hao wa Namibia, Makamu Mwenyekiti wa Chadema, John Heche, amehoji endapo tume hiyo mpya inaweza kupata majibu tofauti na yale yaliyotokea yaliyotolewa na tume iliyotangulia.

Mwanasiasa huyo, ameendelea kuhoji ufanisi wa tume hiyo akisema; "Kama Tume ya Jaji Chande ilishasema kwamba watu wanatekwa kwa sababu ya mapenzi, hii ya sasa itapata wapi ukweli?"

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dkt. Anna Henga, amesema walitarajia ingeundwa tume ya maridhiano ambayo ingeponyesha taifa na siyo Tume ya Jinai.

"Tungeanza na maridhiano halafu ingefuata Katiba Mpya. Tulishagombana, watu wamesikitika, watu wamepata taabu sasa Tume Jinai ni ya nini? Maana tukisharidhiana na kutengeneza Katiba, moja kwa moja tunaingia kwenye taifa lenye furaha," amesema Dkt. Henga.

Akapendekeza kuwa tume hiyo ya jinai sasa iende ikiwa na malengo ya kuponya taifa zaidi, kwa sababu bado ina nafasi ya kuleta maridhiano.



Dkt. Anna Henga

Kwa upande wake, Chama cha ACT-Wazalendo, kimesema hakiitambui tume hiyo kama chombo kinachoweza kutoa uchunguzi unaoaminika.

Katika taarifa yake kwa umma juzi - Jumamosi, chama hicho kimesema kanuni za haki zinataka mtuhumiwa achunguzwe na chombo huru na siyo kujichunguza mwenyewe.

"Muundo wa tume uliotangazwa haujengi imani kwa waathirika, wananchi na jumuiya ya kimataifa kwamba uchunguzi huo utakuwa huru na usio na upendeleo," imesema taarifa hiyo iliyosainiwa na Makamu Mwenyekiti Bara wa chama hicho, Isihaka Rashid Mchinjita.

Chama hicho kimeitaka serikali kuwaachia huru wafungwa wote na watuhumiwa wote wa kesi zenye muktadha wa kisiasa kama njia ya kuelekea kwenye maridhiano ya kweli.

Rais Samia aliunda tume hiyo akitumia mamlaka aliyopewa chini ya Sheria ya Tume za Uchunguzi Sura ya 32 na imepewa miezi mitano kukamilika kazi yake.

Hata hivyo, Rais Samia amesema iwapo kutakuwa na ombi la kuongeza muda, suala hilo litaangaliwa baadaye.

Hivyo, kisheria kuundwa kwa tume hiyo ni utekelezaji wa mamlaka ya rais chini ya sheria hiyo, lakini mjadala wa kisiasa unaendelea kuhusu uhuru, uaminifu na uwezo wa tume hiyo kupata ukweli kuhusu matukio ya Oktoba 2025.

■ Habari

# Ripoti ya LHRC kuhusu haki yaibua mazito



Mussa JUMA, Babati

KITUO cha Sheria na Haki za Binaadamu(LHRC), kimebaini uwepo wa hatari za kimazingira kwa jamii - hasa za asili na mazingira magumu kwa watetezi wa haki za mazingira.

Katika ripoti yake ambayo imepatikana wiki iliyopita – kuna uthibitisho kwamba watetezi wa haki za mazingira katika Mkoa wa Manyara, wana wakati mgumu wa kutekeleza majukumu yao.

Ripoti hiyo ni sehemu ya mradi wa kikanda uliolenga kuimarisha ushiriki wa jamii za asili, asasi za kiraia, mitandao, watetezi wa haki za mazingira katika shughuli za uhifadhi na hatua ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Mradi huo unaotekelezwa katika nchi za Tanzania, Kenya, Uganda kuanzia mwaka 2024-2027 unafadhiliwa na Kituo cha Kimataifa cha Utafiti wa Maendeleo (IDRC).

Miongoni mwa yaliyobainika katika ripoti hiyo iliyowashirikisha watu 504, ni pamoja na uwepo wa athari kubwa za kimazingira ambazo zimetokana na mabadiliko ya tabia nchi, ikiwepo ukame, mafuriko, maporomoko ya ardhi, kuanguka kwa miamba na tope na ukataji miti.

Ripoti hiyo pia imebaini upungufu wa maji, chakula na malisho kwa maeneo ya jamii za asili, ushindani wa matumizi ya ardhi na rasilimali maji kuongezeka, na uwepo wa migogoro baina ya wakulima, wafugaji na jamii nyingine za asili.

LHRC katika ripoti hiyo, imebainisha kuongezeka mazingira ya hatari kwa jamii za asili, vikwazo katika ushiriki wa kiraia inavyoathiri kwa kiwango kikubwa zaidi kwa jamii za wachache na jamii za asili.

Ripoti hiyo, ambayo tayari imekabidhiwa serikali na kwa wadau wa mazingira, pia imebainisha watetezi wa haki za mazingira wanaendelea kukabiliwa na hatari au changamoto mbalimbali wanapotimiza majukumu yao, ikiwepo vitisho, kunyanyaswa, kubughudhiwa kisheria na vitisho dhidi yao na wanafamilia.

Inaendelea Uk. 23

# Wataalamu waonya

Inatoka Uk. 22

Ripoti hiyo imezinduliwa Julai 29, 2026, wilayani Babati na Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Qeen Sendiga na kuhudhuriwa na viongozi wa vijiji kutoka wilaya za Kiteto na Hanang ulipofanyika utafiti huo.

Akizungumza katika uzinduzi huo, mkuu huyo wa mkoa, alipongeza jitihada za LHRC katika masuala ya utetezi wa haki za binadamu ikiwepo haki za mazingira zikiwepo jamii za pembezoni ambazo zipo hatarini zaidi.

Sendika amesema anakubaliana na taarifa za ripoti hiyo za uwepo wa changamoto za kimazingira kutokana na mabadiliko ya tabia nchi, hali ambayo imeanza kuathiri maisha ya wananchi wengi.

Amesema kwa jamii za asili kama Wahadzabe, zinapitia kipindi kigumu, kwani ardhi yao inavamiwa na wakulima na wafugaji, hivyo kuanza kukosa matunda, mizizi na miti ambayo wanaweza kuweka mizinga ili kuvuna asali.

"Mara kadhaa nimetembelea jamii ya Wahadzabe wanalalamikia changamoto za mabadiliko haya ya tabia nchi, lakini siyo jamii hiyo tu, athari za mabadiliko ya tabia nchi ni kubwa kwani hali ya hewa hata hapa Babati mjini imebadilika sana baridi imeongezeka," amesema.

Akielezea ripoti hiyo,Ofisa Utafiti wa (LHRC), Fundikila Wazambi, anasema utafiti huo, umebaini uelewa wa haki za kiraia na haki za mazingira bado ni mdogo katika jamii.

"Ni asilimia 46 pekee ya washiriki walioelekeza kwamba wana uelewa wa kiwango fulani kuhusu haki zao za kiraia huku asilimia 38 tu wakitambua nafasi na mchango wa watetezi wa mazingira"' anasema.

Akizungumzia ripoti hiyo, Mkurugenzi wa LHRC, Wakili Dkt. Anna Henga amesema ripoti imebaini watetezi wa haki za mazingira wana mchango mkubwa katika kulinda rasilimali, kuhimiza uwajibikaji na kuhakikisha mazingira yanalindwa na kutunzwa.

Wakili Dkt. Henga amesema anatoa mwito kwa Serikali ya Tanzania na wadau kuimarisha mfumo wa kisheria na taasisi za ulinzi na utetezi wa mazingira, kukuza ushiriki jumuishi katika uamuzi unaohusu mabadiliko ya tabia nchi, kuimarisha elimu ya haki za kiraia na iwepo wa mfumo madhubuti wa msaada wa haraka kwa wanaokabiliwa na hatari.

Meneja mwandamizi wa Ubora wa Programu (LHRC), Neema Sembeo anasema ripoti hiyo ni muhimu kwa taifa kwani imebainisha changamoto za kimazingira na imekwenda mbali zaidi na kushauri utatuzi.

"Matokeo ya utafiti yameonesha jamii kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabia nchi na kwa watetezi wa haki za mazingira hivyo ni muhimu kuwepo mikakati ya pamoja kukabiliana na changamoto hizi"anasema.

Baadhi ya watetezi wa mazingira walioshiriki utafiti huo; Paulina Lenea na Maingapa Payai wakazi wa Partimbo, Wilaya ya Kiteto, wamesema bila hatua za dharura kuchukuliwa kulinda mazingira na kuwathamini watetezi wa mazingira kutakuwa na athari kubwa.

"Tunapeleka malalamiko kuhusu watu kukata miti na kuharibu mazingira lakini hatua stahiki hazichukuliwi na sisi tunaonekana ni maadui,"amesema Paulina.

Payai amesema kwa sasa jamii za asili ni waathirika wakubwa wa mabadiliko ya tabia nchi kwani ardhi yao inaendelea kuvamiwa na wakulima na watu wanaokata miti na kuchoma mikaa, hivyo muhimu hatua kuchukuliwa.

Mkurugenzi wa shirika la Haliso kutoka Wilaya ya Hanang, ambalo linajihusisha na utetezi wa mazingira, Dominick Dancon anasema kuna umuhimu wa kuimarishwa ushirikiano baina ya watetezi wa mazingira, serikali na wadau wengine kwani lengo lao ni moja kubwa ni kuhakikisha mazingira yanatunzwa kwa manufaa ya sasa na vizazi vijavyo.

Ofisa Miradi wa Shirika la Wanahabari la Usaidizi wa Jamii za Asili (Maipac), Andrea Ngobole amesema ili kuzilinda jamii za asili ni muhimu sasa serikali na wadau wa mazingira kuhakikisha ardhi ndogo iliyobaki ya jamii hizi kulindwa kisheria na kutolewa hati miliki lakini pia kuhakikisha uwepo wa mpango wa matumizi bora ya ardhi vijijini.







Na Loth MAKUZA

# Sifa ya kampuni haipaswi kuachiwa idara moja




KAMPUNI kubwa duniani hazianguki kwa kukosa bidhaa nzuri, zinaanguka kwa kukosa sifa njema. Hilo halibishaniwi.

Tatizo linakuja pale wakuu wa vitengo vya Uhusiano na Umma ya Kampuni wanapoendelea kuzungumza lugha ya vyombo vya habari wakati bodi inataka kusikia lugha ya faida, hasara na hatari. Huko ndiko tofauti inapoanzia.

Takwimu za Taasisi ya Kimataifa ya Wakurugenzi (IoD) na Chama cha Wataalamu wa Uhusiano na Umma nchini Uingereza (CIPR), katika ripoti yao ya mwaka 2022 kuhusu upangaji mkakati na maandalizi ya majanga, zinaonyesha jambo zito.

Kwa miaka minne kati ya mitano iliyopita, ukosefu wa uwakilishi wa wataalamu wa Uhusiano na Umma kwenye ngazi ya bodi umeendelea kuwa miongoni mwa changamoto tano kubwa zinazoikabili taaluma hii.

Hii siyo bahati mbaya, ni matokeo ya jinsi taaluma hii inavyojieleza mbele ya wakurugenzi.

Ripoti ya "PR in the Boardroom" ya Jampuni ya Ambitious PR, ikinukuu Jukwaa la Kiuchumi Duniani (WEF), inasema robo ya thamani ya soko la kampuni inahusiana moja kwa moja na sifa yake.

Hizo siyo takwimu za kupuuza katika chumba cha bodi, hatari ya kutokuwa makini nayo ipo.

Benki ya HSBC ilitozwa faini Uingereza baada ya matangazo yake kuonekana yanapotosha kuhusu mchango wake dhidi ya mabadiliko ya tabianchi, huku yakificha taarifa nyingine muhimu kuhusu uwekezaji wake.

Hiyo ndiyo hatari ya kujipamba kwa lugha nzuri bila vitendo vinavyolingana. Bodi haitaki kusikia lugha nzuri, inataka ushahidi.

Kuhusu vipimo, mfumo unaoitwa Integrated Evaluation Framework, unatoa lugha ambayo bodi tayari inaifahamu kutoka idara nyingine za biashara; pembejeo, matokeo ya kazi, mtazamo uliobadilika, matokeo halisi na mchango wa mwisho kwa biashara (impact).

Bodi haitaki kusikia idadi ya magazeti yaliyoandika habari, inataka kujua tabia ya hadhira imebadilikaje na hilo limeigusaje biashara.

Maandalizi ya majanga

Ripoti ya Taasisi ya Ambitious PR inasisitiza mpango wa dharura lazima uwe sehemu ya mpango wa hatari wa bodi tangu mwanzo, siyo taarifa inayoletwa baada ya moto kuwaka.

Kuna somo jingine, ijapokuwa halitoki kwenye tasnia ya PR moja kwa moja. Kiongozi mmoja wa muundo (design) nchini Marekani, Leonardo De La Rocha, kila Jumatatu huandika upya taarifa ya mkurugenzi mtendaji kwa lugha inayoeleweka na timu yake ya watu thelathini.

Anasema pengo kati ya kile bodi inachokijua na kile timu inachohisi ndicho kinachozalisha uvumi na wasiwasi kazini.

Ndicho hasa kinachotakiwa kufanywa na wakuu wa vitengo wa Uhusiano na Umma kutafsiri, kwa pande zote mbili, kutoka bodi kwenda chini na kutoka chini kwenda kwenye bodi.

Shirley Chisholm, mwanamke mweusi wa kwanza kuchaguliwa Bunge la Marekani, aliwahi kusema kama hawakupi kiti mezani, leta kiti chako mwenyewe.

Ndicho hasa wakuu wa Uhusiano na Umma wanapaswa kufanya, siyo kusubiri mwaliko, bali kujenga thamani inayothibitishwa na namba mpaka kiti kiwe cha kwao kihalali.

Kupanga ni kuchagua; wale watakaobaki kwenye lugha ya zamani ya Uhusiano na Umma watabaki nje ya chumba cha uamuzi.

***Mwandishi wa safu hii ni mtaalamu wa Uhusiano na Umma (PR). Anapatikana kwa namba: 0625 704 995 na kupitia email; projects@ lothmakuza.co.tz***

Na Emmanuel JACOB



# Zaidi ya burudani, michezo ni fursa kwa walemavu

MICHEZO (adaptive sports) siyo burudani tu au njia ya kupoteza muda; ni silaha ya muhimu ya kubadilisha mtazamo wa kijamii, kiuchumi na kisaikolojia kuhusu ulemavu.

Kwa kutumia vifaa vilivyoboreshwa na sheria zilizorekebishwa kama viti vya magurudumu vya mbio, mpira wa miguu wa wasioona (blind football au goalball), au mpira wa wavu wa kuketi michezo hii inavunja vizuizi vya kimwili na kujenga msingi imara wa ukombozi wa kibinadamu.

Mazungumzo yangu na Mkufunzi wa Timu ya Wheelchair Tennis Tanzania wiki hii tukiangazia mafanikio ya watu mbalimbali wenye ulemavu katika mashindano ya kimataifa yalinifanya nipate shauku ya kuandika japo kwa uchache kwa wasomaji wa safu hii kuhusu faida za michezo.

Tafiti za kisayansi, ikiwemo ripoti kutoka Shirika la Afya Duniani (WHO), zinaonyesha kuwa mazoezi ya mara kwa mara hupunguza hatari ya magonjwa yasiyo ya kuambukiza kwa zaidi ya asilimia 30.

Kwa watu wenye ulemavu wa viungo au mfumo wa fahamu, michezo changanifu huongeza uwezo wa mfumo wa mzunguko wa damu (cardiovascular health), kuimarisha misuli, na kuboresha uratibu wa viungo.

Badala ya mwili kuonekana kama chanzo cha ukomo, mchezo unastawisha afya na kujitegemea katika maisha ya kila siku.

Vilevile, utafiti wa hivi karibuni uliochapishwa katika jarida la BMC Public Health unabainisha kuwa kushiriki katika michezo ya walemavu hupunguza kwa kiasi kikubwa viwango vya msongo wa mawazo (depression) na wasiwasi (anxiety), huku ikiongeza kujiamini (self-esteem).

Wanamichezo wanapojifunza mbinu mpya na kushinda changamoto uwanjani, mtazamo wao wa kibinafsi hubadilika kutoka "siwezi" hadi "naweza," jambo linalowapa ujasiri wa kukabili




changamoto za maisha ya kila siku.

Katika jamii nyingi Afrika, unyanyapaa dhidi ya watu wenye ulemavu bado ni changamoto kubwa. Michezo changanifu inatoa jukwaa la kuonyesha uwezo mkubwa wa kiushindani badala ya kuangazia ulemavu.

Wananchi wanaposhuhudia mechi kali za Paralimpiki au mashindano ya kitaifa, mtazamo wa kijamii hubadilika kutoka huruma hadi heshima na uwezeshaji.

Hii inaenda sambamba na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watu Wenye Ulemavu (UN CRPD Article 30), unaosisitiza haki ya kushiriki kikamilifu katika michezo.

Ukisoma na kutafakari kwa makini. Kweli utakubaliana na nami kuwa michezo ni fursa (game changer) kwani inabadilisha dhana ya ulemavu kuwa fursa ya nguvu, ustahimilivu, na usawa.

Ili kutimiza azma hii kikamilifu, serikali na wadau wa maendeleo lazima wawekeze katika miundombinu jumuishi na vifaa nafuu ili kumpa kila mtu fursa ya kushiriki na kujitangaza kimataifa.

***Mwandishi: Emmanuel Jacob, Afisa Mfiziotherapia (Mwenyekiti wa Tanzania Physiotherapy Initiative). Simu: 0765359305 Instagram: Emmanuel Jacob.***

Bustani ya Sheria





Na Wakili Karim Gabriel Mussa

# Sakata la Wakili Fatma Karume – III

KATIKA sehemu ya pili tuliona jinsi Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Tanzania alivyofungua shauri mbele ya Kamati ya Maadili ya Mawakili akiiomba imvue kabisa uwakili Fatma Karume.

Serikali iliwasilisha ushahidi wa maneno aliyotumia mahakamani pamoja na machapisho yake ya Twitter, huku Fatma akisisitiza kuwa alikuwa akitoa maoni ya kitaaluma na kutetea maslahi ya mteja wake.

Sasa ilikuwa zamu ya kamati kutoa uamuzi.

Uamuzi uliotolewa na kamati hiyo uliingia kwenye historia ya taaluma ya uwakili nchini Tanzania.

Je, Tweets zilikuwa za Fatma? Hili ndilo swali la kwanza lililokuwa mbele ya kamati na lilionekana kuwa rahisi kwa sura, lakini zito kwa athari zake.

Je, akaunti ya Twitter iliyowasilishwa ilikuwa ya Fatma Karume?

Je, Fatma alikanusha kuwa baadhi ya machapisho hayo yalitoka kwake. Hata hivyo, Kamati ilichambua ushahidi uliowasilishwa, ukiwemo nyaraka na vielelezo vya video, na ikaridhika kwamba akaunti hiyo ilikuwa yake na kwamba ndiye aliyeandika machapisho hayo.

Kwa hiyo, kamati ikaendelea kujadili maudhui ya maneno hayo.

Je, Fatma alikiuka Maadili ya Uwakili?

Kamati ilikubali kuwa wakili ana haki ya kumtetea mteja wake kwa nguvu zote zinazoruhusiwa na sheria.

Lakini ikasema haki hiyo haimpi wakili ruhusa ya kumshambulia binafsi wakili mwenzake au viongozi wa taasisi za umma kwa lugha inayodhalilisha.

Kwa maoni ya Kamati, kauli za kumuita mwanasheria mkuu kuwa "far too junior," asiye na uwezo na aliyeshindwa kabisa kuishauri serikali hazikuwa hoja za kisheria bali zilivuka mipaka ya maadili ya taaluma.

Kamati ikaongeza kuwa hata kama Fatma alikuwa na maoni kwamba Adelardus Kilangi hakustahili kuwa mwanasheria mkuu, bado alipaswa kuyawasilisha kwa lugha ya kitaaluma inayoheshimu hadhi ya taaluma ya uwakili.

Kamati haikuishia kuangalia maneno yaliyotumika kwenye kesi ya Ado Shaibu pekee, iligundua kuwa wakati shauri la nidhamu likiendelea kusikilizwa kwa siri, Fatma aliendelea kuandika machapisho kwenye Twitter akizungumzia yaliyokuwa yakitokea ndani ya kikao hicho.

Katika baadhi ya machapisho hayo aliikosoa kamati, Mahakama na viongozi wa Mahakama ya Tanzania kwa lugha kali.

Kamati iliona hatua hiyo ilikuwa pia ni ukiukaji wa maelekezo yake pamoja na mwenendo unaodhihirisha kutokuheshimu chombo kilichokuwa kinamsikiliza.

Kamati hata ilibainisha kwamba wakati wa usikilizwaji wa shauri, Fatma aliwahi kuingilia mara kwa mara mwenendo wa kikao na hata kuonyesha kutoridhishwa na namna kilivyokuwa kinaendeshwa.

Kwa mtazamo wa kamati, matukio hayo yaliimarisha hoja kwamba kulikuwa na utovu mkubwa wa nidhamu.

Hukumu ya Kamati

Baada ya kuchambua ushahidi wote, kamati ilifikia hitimisho moja kwamba Fatma Karume alikuwa ametenda kosa kubwa la utovu wa nidhamu wa kitaaluma.

Kwa msingi huo, Kamati ikaamuru jina la Fatma Karume liondolewe kabisa kwenye Daftari la Mawakili (Roll of Advocates) kwa mujibu wa kifungu cha 24 cha Sheria ya Mawakili, 2019.

Kwa lugha nyepesi, Fatma Karume alivuliwa leseni ya uwakili, hivyo kukosa haki ya kuendelea kufanya kazi kama wakili nchini Tanzania.

Uamuzi huo ulitolewa Septemba 23 2020, lakini hapo ndipo vita halisi vilipoanza, kwani Fatma hakukubaliana na uamuzi huo, na badala ya kukata tamaa, alihamishia mapambano yake Mahakama Kuu.

Na huko ndipo alipoibua hoja ya kisheria ambayo iligeuza kabisa mwenendo wa kesi, hoja hiyo haikuhusu kama alitumia lugha nzuri au mbaya.

Ilihusu swali moja muhimu; Je, Kamati ya Maadili ya Mawakili ilikuwa na mamlaka ya kusikiliza shauri lilivyofikishwa mbele yake?

***Mwandishi ni Mwanasheria na Mchambuzi wa Sheria kutoka KGM Attorneys). Anapatikana kwa namba: 0755 395 572 au Email: karimbinmussa@gmail.com***



Na Rashid MTAGALUKA

# Kaulimbiu za Nane Nane zipimwe kwa matokeo

KILA mwaka ifikapo Agosti 8, Watanzania hushuhudia Maonesho ya Kimataifa ya Wakulima (Nane Nane) yakifunguliwa kwa kaulimbiu mpya inayolenga kuhamasisha maendeleo ya kilimo, mifugo na uvuvi.

Kaulimbiu za miaka tofauti zimehimiza matumizi ya teknolojia, kuongeza uzalishaji, kuongeza thamani ya mazao na kutafuta masoko, lakini swali muhimu ni hili; baada ya maonyesho kuhitimishwa, kaulimbiu hizo huendelea kuishi au hubaki kuwa kumbukumbu za hotuba na mabango?

Kaulimbiu ya mwaka huu inayosisitiza uzalishaji wenye tija na upatikanaji wa masoko ni ujumbe unaopaswa kuwahusu Watanzania wote, siyo wakulima, wafugaji na wavuvi pekee. Katika uchumi wa sasa, kila mtu ni mzalishaji wa bidhaa au huduma.

Fundi seremala anatafuta soko la samani zake, mshonaji anahitaji wateja, mwandishi wa habari anauza maarifa yake, msanii anahitaji soko la kazi zake, na mjasiriamali anahitaji wanunuzi wa bidhaa zake. Hivyo, kaulimbiu hiyo ni mwongozo wa uchumi wa kila siku, si wa wiki ya maonesho pekee.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), sekta ya kilimo inachangia takribani asilimia 26 ya Pato la Taifa na inaajiri zaidi ya asilimia 65 ya Watanzania. Takwimu hizi zinaonyesha kuwa maendeleo ya sekta hii yana athari kubwa kwa uchumi wa nchi.

Hata hivyo, changamoto ya masoko bado inaendelea kuwakabili wazalishaji wengi. Mara kwa mara tumeshuhudia nyanya, vitunguu, mahindi na mazao mengine yakiharibika mashambani au kuuzwa kwa bei ya hasara kutokana na ukosefu wa masoko ya uhakika.

Hali hii inaonyesha kuwa uzalishaji pekee hautoshi; soko ndilo linalokamilisha thamani ya jasho la mkulima.

Ndiyo maana kuna haja ya kubadili namna tunavyoangalia kaulimbiu za Nane Nane. Badala ya kuziona kama kauli za msimu, zigeuzwe kuwa dira ya utekelezaji inayopimwa kila mwaka.

Serikali inapozindua kaulimbiu mpya, iwe pia inaweka hadharani tathmini ya kaulimbiu iliyopita. Je, malengo yake yalifikiwa kwa kiwango gani? Ni wakulima wangapi walipata masoko mapya? Ni mazao yapi yaliongezwa thamani? Ni ajira ngapi ziliongezeka kutokana na utekelezaji wa kaulimbiu hiyo?

Bila majibu ya maswali hayo, wananchi watabaki kusikia kaulimbiu mpya kila mwaka bila kuona matokeo yake.

Vilevile, kaulimbiu hizi zinapaswa kuwafikia zaidi vijana. Kilimo cha kisasa siyo jembe pekee, kinahitaji ubunifu, matumizi ya teknolojia, uchakataji wa mazao, biashara mtandao na utafutaji wa masoko ya ndani na nje ya nchi. Hapo ndipo kaulimbiu zinapogeuka kuwa fursa za uchumi badala ya maneno ya maadhimisho.

Nane Nane ni zaidi ya maonyesho, ni jukwaa la kutathmini tulikotoka na kupanga tunakokwenda. Kaulimbiu zitakuwa na maana pale zitakapopimwa kwa matokeo halisi, siyo kwa uzuri wa maneno yake.

Maendeleo ya kilimo hayajengwi na kaulimbiu mpya kila Agosti, bali na utekelezaji unaopimika, unaowajibisha na unaomletea mwananchi kipato na maisha bora.

***Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546 na email; mtagaluka@gmail.com***



Habari




# Ndege inayokaa saa 24 angani yaanza safari

Na Mwandishi WETU

MIAKA kumi iliyopita wakati Shirika la Ndege la Qantas la Australia lilipotangaza kuwa limeanza maandalizi ya kuwa na ndege itakayoweza kuruka angani kwa saa 24, ilionekana kama ndoto ya mwendawazimu.

Lakini baada ya maandalizi, majaribio na uwekezaji katika kipindi hicho, mwezi uliopita – Julai, shirika hilo, kwa kushirikiana na kampuni ya kutengeneza ndege ya Airbus, limetimiza azma hiyo na kuifanya ndoto yake isiwe ya mwendawazimu tena.

Ndoto za shirika hilo ilikuwa ni kuanzisha safari ya moja kwa moja kutoka Australia hadi London, Uingereza na New York, Marekani. Mradi huo ulipewa jina la Project Sunrise.


Julai 24 mwaka huu, ndege ya shirika hilo aina ya Airbus 350-1000ULR ilitua katika Uwanja wa Ndege wa Toulouse, Ufaransa baada ya kuwa angani kwa saa 24 na dakika 24 bila kutua popote ikitokea moja kwa moja Melbourne, Australia.

Hiyo ni safari ya kilometa 23,075, iliyoweka rekodi na kutimiza ndoto ya Qantas ya kuwa na safari ya moja kwa moja ya umbali mrefu.

Ndege hiyo ya majaribio, ambayo ilifika Melbourne ikitokea Toulouse kwa ajili ya safari hiyo, iliondoka majira ya saa 11:27 jioni. Ilikuwa imepangiwa kufanya safari hiyo kwa kuzunguka Bahari ya Pacific badala ya kutumia njia ya Bahari ya Hindi kama ilivyotumia wakati inakwenda Melbourne.

Ndege hiyo ilikatiza mabara matatu na bahari kubwa mbili kabla ya kutua. Kabla ya safari hiyo rasmi ya majaribio, ndege hiyo iliondoka Toulouse kuelekea Melbourne kupitia Asia na kutumia saa 19 angani. Ukiziweka safari hizo mbili; Toulouse - Melbourne iliyochukua saa 19 angani na Melbourne- Toulouse, ni kama ndege hiyo iliizunguka dunia.

Inaendelea Uk. 19



# Ndege inayokaa saa 24 angani yaanza safari

Inatoka Uk. 18

Marubani kutoka mashirika ya Airbus na Qantas walihusika katika safari hiyo ya majaribio ambayo imefungua milango ya kuwepo kwa safari kama hizo na hivyo kupunguza muda wa safari na usumbufu ambao abiria wanaosafiri umbali mrefu wanaupata kwa kutumia ndege zinazokuwa na vituo kadhaa njiani.

**Project Sunrise ni nini?**

Huu ni mradi uliobuniwa na Shirika la Ndege la Qantas ukilenga kuanzisha safari ndefu za ndege kutoka Sydney hadi London na New York.

Ili kutimiza mradi huu, Qantas imepanga kutumia ndege 12 aina ya A350-1000ULR, ambazo ni maboresho ya ndege aina ya Airbus 350, ambazo zimetengenezwa mahsusi kuweza kumudu safari hiyo.

Ili kuhakikisha kuwa ndege hiyo inaweza kumudu mikikimikiki ya safari hiyo ndefu na abiria wanakuwa katika hali nzuri, Airbus imelazimika kuifanyia marekebisho kadhaa ndege aina ya Airbus 350.

Kwanza, ndege hii itakuwa na tanki la mafuta lenye uwezo wa kuhifadhi lita 20,000 za mafuta ambayo yanaiwezesha kufanya safari hiyo ndefu bila kulazimika kuongeza mafuta, ikiruka kwa zaidi ya saa 24 angani.

Pia, idadi ya siti katika ndege hii mpya imepunguzwa kutoka 297 ambazo ni kawaida kwa ndege a aina hiyo hadi siti 238.

Abiria anapoingia ndani ya ndege hii anaanza kuona tofauti anapofika mlangoni kutokana na chumba cha kukaribisha abiria kuwa na aina maalum ya taa.

Siyo hapo tu, hata kwenye ndani ya ndege kuna aina tofauti za taa zikiwa zimetengenezwa kuakisi majira tofauti ya siku.

Zipo taa zinazoakisi nyakati mbalimbali za siku kama vile asubuhi, mchana, jioni, adhuhuri, usiku na alfajiri. Hii yote ni kumfanya abiria asijisikie kuwa nje ya mazoea yake ya jinsi siku inavyokwenda akiwa ndani ya ndege hiyo.

Taa hizi huweza kuakisi muda na majira halisi ya dunia kulingana na safari inavyoendelea.

Kwa ujumla kuna aina 12 tofauti za taa ndani ya ndege hii.

Kazi ya kupata aina ya taa hizo ilihusisha pia watafiti nguli kutoka Chuo Kikuu cha Charles Perkins Centre na Caon Design Office, Ausralia.

Baada ya utafiti mpana na majaribio kwa saa 150, timu hii ilipata aina ya taa zinazopaswa kuwemo kwenye ndege hiyo ili kukidhi kile ambacho Qantas ilikuwa inataka kitokee.

Pia, kila aina ya mwanga wa taa unamfanya abiria aendane na mabadiliko ya time zones kabla hajatua.

Aidha, kuna mabadiliko makubwa kwenye siti kwani zimetengenezwa kumfanya abiria asichoke sana akiwa amekaa kwa muda mrefu.

Sehemu ya daraja la juu lina siti ambazo zinaweza kukunjuka na kuwa kama kitanda chenye godoro na kumwezesha abiria kulala. Chumba hiki cha daraja la juu pia kina kabati la nguo!

Pia ndege hiyo imeongezewa eneo maalum katikati ambapo kuna kituo cha viburudisho. Eneo hili linaruhusiwa kutumiwa na kila abiria aliye ndani ya ndege.

Katika eneo hili abiria wanaruhusiwa kuzunguka zunguka wakinyoosha viungo baada ya kukaa au kulala kwa muda mrefu.

**Safari zitakavyokuwa**

Baada ya majaribio, shirika hilo limepanga kuanza safari za abiria kuanzia Oktoba mwaka huu, safari ya kwanza itakuwa ni kutoka Australia hadi London.

Safari hii ya moja kwa moja itapunguza muda wa safari kwa saa nne kulingana na muda unaotumiwa na ndege zinazolazimika kusimama njiani zinaposafiri kati ya miji hiyo miwili.

Safari inayofuata itakuwa ni ya Sydney hadi New York itakayoanza mwakani.

Bado Shirika la Qantas halijawa na mpango wa kuongeza maeneo ambayo yatahudumiwa na ndege hiyo ya masafa marefu.

# Barua za Wasomaji



## Tunakaribisha barua. Tuma kupitia

**Tuandikie kero ya eneo lako kupitia WhatsApp namba; +255 712 792216 au tutumie kupitia email; info@pambazuko.or.tz**

## Tutaandamana kwenda Dawasa kudai maji

**Mhariri,**
SISI wananchi wa mitaa ya Masaki, Amani na Kilima Cheupe-Mbezi Kimara, Dar es Salaam, tumekosa maji kwa zaidi ya miezi sita.

Tumechoka kuahidiwa uongo wa mara kwa mara na mafundi wa Dawasa, ambao kila wakifika eneo hili wanadai wanashughulikia tatizo kumbe hakuna kitu.

Kwa kipindi kirefu tumeishi kwa kununua maji ambapo ndoo inauzwa shilingi 500 na kutumia maji ya mabawa ambayo siyo salama, ambayo yameleta shida kubwa kwa familia zetu kupata magonjwa ya tumbo.

Sasa tumeamua tuandamane kwenda ofisi ya Dawasa, tukakutane na uongozi watuambie suluhisho la kudumu la tatizo letu ni nini na litapatikana lini. Tumechoka, na kama tumetengwa basi waje waondoe mabomba yao tujue hatuna maji.

Tumepanga kuandamana kwenda ofisi za Dawasa Kinyerezi muda wowote kuanzia sasa.

**Innocent Frank,**
**Masaki, Mbezi**

## Nini tatizo Barabara Mailimoja – Baobab

**Mhariri,**
HII ni mara ya nne naleta tena kero kuhusu barabara inayotoka Mailimoja hadi Baobab kuelekea Bagamoyo kupitia Kata ya Pangani, Halmashauri ya Kibaha Mji.

Barabara hii ni mbovu kupindukia.

Ahadi zimekuwa nyingi kuwa tungejengewa kwa kiwango cha lami tangu mwaka juzi lakini hakuna kinachoendelea.

Tunaomba kwa mara nyingine mamlaka itutatulie kero hii.

**Anna Rweyemamu,**
**Kibaha.**
**0783682018**

## Walimu washirikiane na wazazi

**Mhariri,**
NAANDIKA barua hii ili kutoa wasiwasi wangu kuhusu tatizo linaloongezeka la wanafunzi wengi kuchelewa kufika shule kila siku.

Kuchelewa kunapunguza muda wa kujifunza. Mwanafunzi anayekosa masomo ya mwanzo hukosa misingi muhimu.

Hii inachangia kupata alama duni na hata kushindwa mitihani.

Pia tabia ya kuchelewa inaharibu nidhamu, shule inafundisha uongozi wa muda na uwajibikaji.

Mwanafunzi anayezoea kuchelewa anakuwa mtu asiyejali muda, jambo ambalo litaathiri maisha yake baadaye.

Pia usalama unakuwa hatarini, wanafunzi wengi hukimbia barabarani au kutumia njia za mkato ili kuwahi kufika shuleni, hivyo kuhatarisha maisha yao.

Tatizo hili linatokana na wazazi kutowaamsha watoto mapema au wanafunzi wenyewe kushindwa kuwajibika kwa hilo, lakini pia msongamano wa magari na baadhi ya wanafunzi kukosa nidhamu binafsi.

Napendekeza shule zishirikiane na wazazi kutoa elimu ya umuhimu wa muda na serikali iboreshe usafiri wa asubuhi.

Tujadiliane ili kizazi chetu kipate elimu kamili bila vikwazo vya ucheleweshaji.

**Mwanahamisi Mwenda,**
**Ilala, Dar es Salaam.**


MOVE FOR DISABILITY
INCLUSION BY DESIGN 26'
WALK
with Us
29th August 2026
SPONSERED BY circleg
Kua mshiriki kwa Tshs 40,000/- Tu!
Nunua ticket yako kutumia Lipa Namba
MOVE FOR DISABILITY
6 1 2 4 6 6 1 0
INCLUSION BY DESIGN 26'
SPONSERED BY
UHURU
circleg
Pambazuko

## Wazo Binafsi

# Ya Rwanda yapaswa kuigwa Tanzania kunusuru vijana



*Rais wa Rwanda, Paul Kagame*

**Na Hellen NGOROMERA**

KILICHOFANYWA na Serikali ya Rwanda wiki iliyopita kupiga marufuku baadhi ya pombe kali kusambazwa na kuuzwa nchini humo, kinawahusu zaidi vijana Tanzania.

Ongezeko la matumizi makubwa ya vileo vikali miongoni mwa vijana nchini limekuwa tishio kubwa kwa afya ya umma, maendeleo ya taifa na maadili ya jamii.

Takwimu za Wizara ya Afya zinaeleza kuwa zaidi ya asilimia 35 ya vijana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 24, wamewahi kutumia pombe kali angalau mara moja.

Vinywaji vyenye kiwango kikubwa cha kilevi vimekuwa vikitumiwa kwa wingi na vijana katika miji mikubwa na vijijini.

Sababu za msingi zinazochangia ongezeko hilo ni pamoja na shinikizo la rika, katika jamii ya sasa, vijana wengi huona matumizi ya vileo kama ishara ya ukomavu na hivyo kushindwa kujizuia kwa hofu ya kubaguliwa.

Hali hutokea sana pale ambapo kijana akimuona mwenzake – wa rika moja, akitumia kilevi naye kujiuliza; "kama huyu anafanya hivi na huyu ni sawa na mimi, kwa nini mimi nibaki nyuma?"

Iwapo swali hili halitakuwa na tafakuri nzuri nyuma yake, bila kujua au kutarajia, kijana anaweza kujikuta ametumbukia kwenye unywaji wa pombe wenye madhara.

Aidha, changamoto za kiuchumi kama ukosefu wa ajira na umaskini pamoja na shinikizo la masomo zimesababisha baadhi ya vijana kutumia pombe kama njia ya kukwepa uhalisia.

Pia upatikanaji rahisi wa vileo hivyo, tena kwa bei ndogo, umerahisisha hata wanafunzi kuthubutu kuvitumia!

Mitandao ya kijamii ambayo kwa kiasi kikubwa imekuwa ikihusisha matumizi ya vileo na mafanikio na starehe, vijana wengi huvutiwa na kuamua kuonja vileo.

Wataalamu wa afya wamekuwa wakieleza madhara ya matumizi ya vinywaji vikali kuwa ni kuharibu viungo muhimu vya mwili ikiwamo ini na figo na kuongeza hatari ya kupata magonjwa ya muda mrefu kama kisukari, vidonda vya tumbo na saratani.

Kielimu, wanafunzi wengi wamekuwa wakipata matokeo duni na hata kusimamishwa masomoni kutokana na tabia ya ulevi.

Kijamii, vileo vikali vimekuwa chanzo kikubwa cha migogoro ya familia, vurugu, ajali za barabarani na uhalifu.

Ripoti za vyombo vya dola zinaonyesha kuwa zaidi ya asilimia 40 ya matukio ya kihalifu yanayofanyika usiku, yanahusiana moja kwa moja na ulevi.

Kisaikolojia, matumizi ya muda mrefu ya vinywaji vikali husababisha uraibu ambapo mtu anaishia kunywa si kwa raha bali ili kuepuka dalili za kujiondoa. Hali hii huambatana na mfadhaiko na mawazo ya kujidhuru au hata kujiua.

Ili kukabiliana na changamoto mbalimbali kunahitaji jitihada za pamoja; serikali inapaswa kuimarisha utekelezaji wa sheria na kanuni zinazodhibiti uuzaji holela wa vileo.

Taasisi za elimu na kidini nazo zina wajibu wa kutoa elimu ya kina kwa vijana kuhusu madhara ya vileo hivyo pia ni muhimu kuwepo kwa programu za kuwajengea vijana stadi za kujiajiri na kuwapa fursa za michezo na sanaa ili wawe na namna mbadala ya kutumia muda wao.

# Mizani ya uhuru wa uchumi haupimi kwa kiwango cha misaada pekee

Na Steven MBOGO

PROFESA Kitila Mkumbo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji), amesema kuwa Tanzania imepunguza kwa kiwango kikubwa utegemezi wa misaada ya nje, hivyo kusitishwa au kuwekwa masharti kwenye misaada hakutakuwa na athari kubwa kama ilivyokuwa zamani.

Anasema masharti ya misaada hayana tena athari ya kimkakati katika uamuzi wa serikali, kwani tayari imejumuisha hatari ya kupungua au kusitishwa kwa misaada hiyo katika mfumo wake wa usimamizi wa fedha za umma.

Pia alieleza kuwa utegemezi wa misaada katika bajeti ya serikali umeshuka kwa kiwango kikubwa katika miaka ya karibuni, kwamba serikali imeendelea na sera ya kuongeza mapato ya ndani na kujitegemea katika kugharamia maendeleo, hivyo nafasi ya misaada kwenye bajeti imeendelea kupungua.

Kauli ya Prof. Kitila Mkumbo inaweza kuchambuliwa kwa jicho la sera za uchumi wa kimataifa bila kuikataa au kuikubali moja kwa moja.

Hoja kuu siyo misaada imepungua, bali kama Tanzania imejenga kiwango cha juu cha uhimilivu wa uchumi, kinachoweza kuhimili misukosuko ya nje bila athari kubwa.

Kwa mtazamo wa uchumi wa kimataifa, utegemezi wa misaada ni kipimo kimoja tu cha uhuru wa kiuchumi.

Hivi sasa nchi nyingi hazidhibitiwi tena kupitia misaada pekee; ushawishi umehamia katika masoko ya fedha, uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje (FDI), mikopo ya mashirika ya fedha ya kimataifa, teknolojia, minyororo ya thamani duniani, mifumo ya malipo ya kimataifa, na upatikanaji wa masoko ya kimataifa.

Hivyo, hata kama misaada inapungua, hilo pekee halimaanishi kuwa uwezo wa nje wa



Prof. Kitila Mkumbo

kuathiri uchumi wa taifa umepungua kwa kiwango hicho hicho.

Aidha, historia ya uchumi wa dunia inaonyesha kuwa vikwazo vya kisasa havijikiti tena katika kusimamisha misaada. Mara nyingi hulenga upatikanaji wa mitaji, uwekezaji, huduma za kifedha, uhamishaji wa teknolojia, au imani ya wawekezaji.

Katika mazingira hayo, kauli kwamba “vikwazo vya misaada haviwezi kufanya kazi tena” inaweza kuwa sahihi katika muktadha mwembamba wa misaada, lakini siyo lazima iwe sahihi katika maana pana ya shinikizo la kiuchumi la kimataifa.

Inaendelea Uk. 34

Makala

# Mizani ya uhuru...

Inatoka Uk. 33

Pia, uhuru wa kiuchumi haupimwi kwa kiwango cha misaada pekee, bali kwa uwezo wa taifa kugharamia matumizi yake kupitia mapato ya ndani, kuwa na msingi mpana wa kodi, sekta binafsi yenye ushindani, uzalishaji wenye thamani ya juu, na uwezo wa kuuza bidhaa na huduma zenye ushindani katika soko la dunia.

Bila misingi hiyo, kupungua kwa misaada kunaweza kuwa matokeo ya mabadiliko ya sera za wafadhili badala ya ushahidi wa kujitegemea kikamilifu.

Kwa upande mwingine, ikiwa serikali imejumuisha hatari ya kupungua kwa misaada katika mfumo wa usimamizi wa fedha za umma, hiyo ni hatua ya usimamizi wa hatari.

Lakini usimamizi wa hatari hauondoi hatari yenyewe; unasaidia kujiandaa nayo. Hivyo kauli hiyo haipaswi kutafsiriwa moja kwa moja kuwa uchumi sasa hauwezi kuathiriwa na shinikizo za nje.

Katika muktadha wa kimataifa, nchi zinazotajwa kuwa na uhuru mkubwa wa kiuchumi, kama vile Korea Kusini, Singapore, au Norway hazikufikia hatua hiyo kwa sababu ziliondoa utegemezi wa misaada pekee, bali kujenga taasisi imara, kuongeza tija ya uzalishaji, kuwekeza katika elimu na teknolojia, kuboresha utawala wa sheria, na kuifanya sekta binafsi kuwa injini ya ukuaji wa uchumi.

Hivyo, kipimo cha kweli cha kujitegemea ni uwezo wa uchumi kuendelea kukua, kuvutia uwekezaji, na kustahimili mishtuko ya dunia bila kutegemea hatua za dharura.

Kwa hiyo, swali la msingi siyo kama misaada imepungua, bali – Je, Tanzania imejenga uchumi unaoweza kustahimili mabadiliko ya masoko ya dunia, kupungua kwa uwekezaji wa nje, mabadiliko ya bei za bidhaa, na misukosuko ya kifedha ya kimataifa bila kuyumba?

Hicho ndicho kipimo kinachotumiwa na wachumi wengi duniani kutathmini kiwango halisi cha mamlaka ya kiuchumi.

Kwa mtazamo huo, kauli ya Prof. Kitila inaweza kueleweka kama ujumbe wa kisiasa na kiutawala kuhusu maendeleo ya usimamizi wa fedha za umma.

Hata hivyo, kutoka katika uchambuzi wa uchumi wa kimataifa, ni hitimisho pana linalohitaji kuungwa mkono na viashiria vinavyoonyesha uwezo wa uchumi wa taifa kujitegemea katika uzalishaji, mapato ya ndani, ushindani wa kimataifa, na ustahimilivu dhidi ya shinikizo mbalimbali kutoka nje.

***Mwandishi ni mtafiti, mchambuzi na msomaji mkubwa wa Pambazuko***



# eSwatini yenye tabasamu inavyoficha sura ya hofu

IDADI kubwa ya watu huitazama na kuipa tafsiri eSwatini kupitia nyuso tatu zenye tabasamu; Mfalme Mswati III, Mama Malkia LaTfwala na Waziri Mkuu Russell Dlamini.

Nyuma yao kuna milima ya kijani, mabonde yenye kuvutia na mandhari tulivu yanayoifanya nchi hiyo ionekane kama kisiwa cha amani kusini mwa Afrika.

Taswira hiyo huvutia karibu watalii 800,000 kwa mwaka. Wageni, wakiwamo viongozi wa mataifa mbalimbali, hupokewa kwa bashasha na kuonyeshwa uzuri wa ufalme huo.

Hata uamuzi wa Mfalme Mswati wa kubadili jina la nchi kutoka Swaziland kwenda eSwatini mwaka 2018, uliwasilishwa kama kurejesha hadhi na utambulisho wa asili.

Lakini ukitazama nyuma ya tabasamu, milima na sherehe za kifalme, unaiona nchi nyingine; taifa lililofunikwa na hofu, ukimya, umaskini na mamlaka yasiyopingwa.

Chanzo kimoja kilimweleza mwanasayansi wa siasa, Nqobile Mkhatshwa kuwa serikali imejenga hofu, kisha ukimya unaotokana na hofu hiyo hutafsiriwa kwa makusudi kama furaha na amani ya wananchi.

Jeraha la mwaka 2021

Sura hiyo ilijitokeza wazi Juni 2021, maandamano yalipozuka kutokana na kupanda kwa gharama za maisha, upungufu wa walimu na matumizi makubwa ya viongozi.

Serikali ilijibu kwa nguvu ya dola na kusababisha mtu wa kwanza kuuawa Juni 29, na baadaye zaidi ya watu 60 waliripotiwa kupoteza maisha.

Hadi leo, mauaji hayo hayajadiliwi kwa uwazi na hakuna uwajibikaji unaoonekana.

Baada ya umwagaji damu, mhariri mmoja, Bheki Makhubu alisema hakuna mtu aliyethubutu tena kupaza sauti.

Wabunge hawa; Magawugawu Simelane, Bacede Mabuza na Mthandeni Dube walipoibua suala hilo, waliondolewa bungeni.

Simelane alikimbilia uhamishoni, huku Mabuza na Dube wakifungwa. Mabuza anatumikia kifungo cha miaka 25 na ameeleza hofu kuhusu usalama wake gerezani.




Kiongozi wa chama cha People's United Democratic Movement, Mlungisi Makhanya, naye aliripotiwa kunusurika jaribio la kuuawa akiwa uhamishoni.

Mwanzoni mwa maandamano, huduma ya intaneti ilizimwa kwa saa 216. Kampuni ya MTN ilishutumiwa kwa kushirikiana na serikali, ingawa haikuwajibishwa.

Tume ya Kimataifa ya Wanasheria iliita hatua hiyo "isiyokuwa ya lazima na isiyolingana na hali," ikikadiria kuwa uchumi ulipoteza dola milioni 15.8.

Wachache matajiri, shida za wengi

Mgongano kati ya tabasamu la dola na maisha ya wananchi unaonekana pia katika uchumi.

Mwaka huu, wabunge waliongezewa mishahara kwa asilimia 54, na kufikisha malipo yao zaidi ya Rand milioni moja kwa mwaka. Kiasi hicho ni sawa na Shilingi za Tanzania milioni 162.

Wakati huo, watumishi wa umma waliachwa bila nyongeza na kulazimika kuandamana.

Waziri Mkuu Dlamini mwenyewe amekiri kuwa theluthi mbili ya wananchi wanaishi chini ya mstari wa umaskini. Chini ya Shilingi 3,000 za Tanzania kwa siku.

Inaendelea Uk. 36

Makala ya Kimataifa

# Mizani ya uhuru...

Inatoka Uk. 35

Elimu na afya zinaendelea kukabiliwa na uhaba wa fedha, huku matumizi ya dola na vyombo vya usalama yakipewa uzito.

Sikhumbuzo Thomo wa Swaziland Solidarity Network anasema kila fedha inayoongezwa kwa vikosi vya usalama inapunguza fedha za zahanati, vitabu vya shule na maafisa ugani wanaohitajika kuongeza uzalishaji wa wakulima.

Mfumo wenyewe unaendeleza pengo hilo. Seneti yenye wajumbe 30, ambao wengi huteuliwa na mfalme, inaweza kuzuia uamuzi wa wawakilishi waliochaguliwa. Hivyo swali linabaki; taasisi hizo zinawatumikia wananchi au kulinda mfumo wa kifalme?

**Amani yao, hofu inayoishi**

Mfalme Mswati anaendelea kuhubiri amani, lakini wanaharakati wanasema kauli hiyo inalenga kuipamba nchi mbele ya jumuiya ya kimataifa.

Rais wa Umoja wa Kitaifa wa Wanafunzi wa Swaziland, Vusi Simelane, anayeishi uhamishoni, amesema Waswazi wametekwa, kufungwa, kulazimishwa kukimbia na hata kuuawa.

Kisa kinachobeba uzito mkubwa ni mauaji ya wakili wa haki za binadamu na mwandishi wa habari Thulani Maseko. Januari 2023, Maseko alipigwa risasi mbele ya familia yake, muda mfupi baada ya mfalme kutoa kauli kali dhidi ya waliohusishwa na machafuko.

Mjane wake, Tanele Maseko, amesema anaamini mfalme anajua aliyehusika. Hakuna jibu la kuridhisha lililotolewa kuhusu mauaji hayo.

Maseko – kupitia uwezo wake mkubwa wa kuandika na kuzungumza, alipendwa na kufuatiliwa na wengi. Alikuwa akihamasisha mazungumzo ya kitaifa.

Rais wa Afrika Kusini Cyril Ramaphosa na Mswati waliwahi kukubaliana kuwa sekretarieti ya kikanda isaidie kuanzisha jukwaa la kuleta maelewano, lakini juhudi hizo zimefifia.

Mfalme hajakutana hadharani na waathirika au familia za waliouawa mwaka 2021.

Kwa utamaduni wa Waswazi, kiongozi wao anapaswa kuwa mlinzi wa watu wake, syo mtawala anayewaacha na majeraha yasiyoponywa.

Afrika inayotazama pembeni

Ukimya wa majirani nao unaisaidia eSwatini kuficha hali yake. Viongozi na mabalozi wa Afrika huahidi kuendeleza ushirikiano na serikali bila kugusia ukiukwaji wa haki za binadamu.

Mwandishi wa habari za uchunguzi, Zweli Dlamini anaamini washirika wa Mswati wanapuuza ukatili kwa sababu ya maslahi yao ya kisiasa na kiuchumi.

Ndani ya nchi, vyama vya siasa vimepigwa marufuku, vyama vya wafanyakazi na harakati za wanafunzi vimebaki nguzo kuu za kudai demokrasia, lakini hukabiliwa na vikwazo.

Serikali ilipiga marufuku maandamano ya Mei Mosi, na mwanaharakati aliyekamatwa kwa kuvaa fulana yenye kuhamasisha amani na mabadiliko, alifariki kizuizini; serikali ikadai alijiua.

Pamoja na mambo mengine, wanaharakati wan chi hiyo wamekuwa wakiishutumu serikali kwa kutoa pasipoti za kidiplomasia kwa mhubiri Uebert Angel na mfanyabiashara Wicknell Chivayo, ambao siyo Waswazi.

Maswali zaidi yaliibuka baada ya eSwatini kupokea wafungwa 11 kutoka Marekani katika makubaliano yaliyoelezwa kuwa na thamani ya dola milioni 5.1.

Waziri Mkuu Dlamini anasisitiza kuwa wananchi wanapendelea mfumo wa uongozi wa Tinkhundla.

Mfumo huo ulianzishwa mwaka 1973 na Mfalme Sobhuza II baada ya kuvunja Katiba, kufuta vyama vya siasa na kujikusanyia mamlaka makubwa ya kiutendaji, kisheria na kimahakama.

Hata hivyo, utafiti wa Chuo Kikuu cha Swaziland unaonyesha kuwa wanaotaka ubadilishwe ni wengi kuliko wanaoouunga mkono.

Hiyo ndiyo eSwatini inayofichwa na tabasamu la kifalme, mandhari ya milima na lugha ya amani.

Nje, ni ufalme mtulivu unaowakaribisha watalii; ndani, ni jamii inayozuiwa kuzungumza, kuandamana na kuamua mfumo wa utawala inaoutaka.

Mpaka hofu itakapoondolewa, haki kutendeka na wananchi kuruhusiwa kushiriki kikamilifu, picha inayouzwa duniani itaendelea kuwa pazia linalofunika uhalisia mchungu.

***Mwandishi anaishi Afrika Kusini na imetafsiriwa na Pambazuko kwa ombi lake.***

# Habari katika Picha

*Kutokana na ongezeko kubwa la matumizi ya gesi kwa vyombo vya moto na vituo vya kutolea huduma hiyo kuwa vichache kunawasababisha madereva wa Bajaji kukaa kwenye foleni kujaza gesi kama walivyoshuhudiwa katika Kituo cha Mlimani kilichopo Marabara ya Sam Nujoma, jijini Dar es Salaam jana. Picha na Pambazuko.*






*Kamishna wa Kamisheni ya Uchunguzi wa Sayansi ya Jinai, CP Shabani Hiki, akipokea Hati ya Shukrani kutoka Umoja wa Vijana wenye Ualbino Tanzania (TYAF) kwa niaba ya Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Camillus Wambura, kwa kutambua jitihada za Jeshi la Polisi katika kulinda usalama wa raia na mali zao, jijini Dar es Salaam. Picha na Jeshi la Polisi*




*Mwenyekiti wa Tume ya Rais ya Uchunguzi wa ghasia za Oktoba 29 mwaka jana, Jaji Shabani Liila (kushoto), akiwa na wajumbe wa tume hiyo, Jaji Petrus Damaseb kutoka Namibia (katikati) na Jaji Barishaki Cheborion (Uganda) wakati wa uzinduzi wa tume hiyo, Ikulu, jijini Dar es Salaam. Picha na Ikulu.*




*Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na Rais wa Uganda, Yoweri Museveni, wakishuhudia utiaji saini Hati ya Makubaliano kuhusu mapendekezo ya kuendeleza Kituo cha Nishati cha Kikanda mkoani Tanga. Hafla hiyo ilifanyika katika viwanja vya Ikulu, jijini Dar es Salaam juzi. Picha na Ikulu.*



*Baadhi ya wakazi wa Masaki, Mbezi kwa Musuguri jijini Dar es Salaam wakichota maji yanayovuja kutoka kwenye mabomba. Wakazi hao wanlazimika kufanya hivyo kwa sababu maji hayo hayafiki kwenye makazi yao kwa kipindi kirefu cha zaidi ya miezi sit ana kulazimika kutumia maji ya bwawa ambayo si salama kwa afya zao. Picha na Pambazuko.*



Na Anti MSHAURI







# Siri yako ni mali yako

HABARI za wiki hii msomaji wangu wa safu ya uhusiano. Karibu tushiriki elimu na ushauri kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu eneo hilo.

Leo nitaeleza umuhimu wa kutomshirikisha rafiki mambo yako ya ndani.

Urafiki ni mzuri na hakika ni baraka, lakini siyo kila mlango wa moyo wako unapaswa kuwa wazi kwa kila mtu.

Leo watu wengi wameumizwa na rafiki wa karibu.

Kuna unayemwambia ndoto yako na kesho yake ndoto hiyo ikawa utani wa mtaa.

Mwingine unaweza kumwambia shida ya kifedha na wiki moja baadaye ikawa soga mezani kwa watu wasiomhusu.

Mwingine unaweza kumwamini na kumpa namba za siri ya akaunti yako na baada ya muda ukaibiwa.

Hili linatokea kwa sababu tatu kuu; kwanza kuna watu ambao kinywa chao hakiwezi kukaa kimya. Unachokwambia leo kwa siri, kesho kinaweza kuenea kwenye vikundi vya WhatsApp, TikTok na kwingine.

Jambo jingine ni wivu; hapa unaweza kukuta rafiki anayejua maendeleo yako akatabasamu na wewe, lakini moyoni akatamani usiendelee na wakati mwingine akijua mipango yako yote mikubwa anaweza kuikwamisha kimya kimya bila wewe kujua.

Pia kuna suala la ugomvi; inawezekana leo akawa rafiki na kesho mkawa maadui na ile habari uliyompa wakati mkiwa mmeshibana kwa uaminifu inageuka kuwa silaha ya kukupiga.

Hii haina maana kuwa na shaka na watu wote au kuishi kama kifungoni. Kuna mambo yako ambayo si lazima kila mtu ayajue. Mipango yako ya kifedha, udhaifu wako wa ndani, na siri za familia yako ni mali binafsi. Mpe mtu kiasi cha imani anachostahili, usimpe kila kitu.

Mjaribu kwanza na mambo madogo. Kama hawezi kuyahifadhi, basi usimpe makubwa.

Kumbuka kanuni moja; maji yakimwagika hayazoleki. Neno likitoka kinywani mwako halirudi. Linda amani yako kwa kujua pa kusema na pa kukaa kimya.

Urafiki wa kweli hauvunjiki kwa sababu umeka kimya. Badala yake unaimarika zaidi kwa sababu una mipaka na heshima.

Linda hekima yako, linda siri yako na hakikisha urafiki wako na mwingine unakuwa na mipaka

Tukutane wiki ijayo.

***Kwa maoni na ushauri: hellen2ngoromera@gmail.com Au simu: 0715 88 67 49.***

# Pochi, mkoba vinavyoongeza mvuto wa mavazi



KATIKA suala la mitindo na utanashati, ubunifu ni jambo muhimu zaidi kwa kuwa ndiyo kigezo pekee kinachoweza kumtofautisha mtu mmoja au mwingine.

Katika hili, kila mwanamke anapaswa kuwa mbunifu ili kuleta vitu tofauti toafuati ambavyo kwa namna moja au nyingine itaibua mitindo mipya.

Leo katika safu hii nitazungumzia namna pochi au mkoba vinavyoweza kuongeza mvuto kwa mwanamke.

Pochi au mkoba inaweza kuonekana ni kwa ajili ya kubebea vitu vidogo vidogo, anavyopaswa kuwa navyo mwanamke, lakini wengi hawafahamu kuwa vinachangia kuongeza mvuto katika mavazi.

Kwa kulinganisha na rangi zinazoshabihiana na nguo au viatu ulivyovaa, mkoba au pochi inaweza kuonekana zaidi na kuvutia katika macho ya mtu anayekutazama.

Hivyo unavyopigilia mavazi yako zingatia na aina ya rangi ya pochi unayoibeba.

## Utunzaji nywele za asili



NYWELE za asili ambazo hazijawekwa dawa zikitunzwa vizuri huwa zinapendeza na kuvutia zaidi.

Jambo moja kubwa unalopaswa kuzingatia katika utunzaji wa nywele zako za asili; kwanza hakikisha unaziosha kwa kutumia shampoo zilizotengenezwa kwa ajili ya nywele zisizo na dawa.

Pia unapaswa kupaka mafuta ya maji ili kuleta unyevunyevu na nywele kung'aa. Unaweza kutumia mafuta ya nazi, nyonyo au zaituni.

Mafuta hayo husaidia kulainisha ngozi ya kichwa kufanya nywele kuwa vizuri na kuzuia mba kichwani na kuepuka nywele kuwashawasha.

Epuka kutumia mafuta ya mgando maana hutengeneza mba kichwani kwenye nywele za asili ambayo husababisha miwasho.





# Sugu awataka wasanii kuwekeza

Na Mwandishi WETU

MWANAMUZIKI mkongwe wa Hip Hop nchini, Joseph Mbilinyi maarufu Sugu, amewataka wasanii kutumia umaarufu wao kuanzisha na kukuza biashara badala kutegemea sanaa pekee.

Sugu ambaye pia ni mwanasiasa na mfanyabiashara, ametoa rai hiyo juzi jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa duka lake la kubadilisha fedha za kigeni aliyoipa jina la Desderia Bureau de Change.

"Wasanii, wanamichezo na watu wote maarufu wanapaswa kutambua kuwa majina yao ni mtaji…"

"Wakiyatumia vizuri wanaweza kuanzisha biashara mbalimbali na kujitengenezea fursa za maendeleo badala ya kutegemea umaarufu pekee," amesema Sugu.

Amesema kuanzishwa kwa Desderia Bureau de Change ni sehemu ya juhudi zake za kuwekeza katika sekta rasmi ya biashara na kuhamasisha watu wengine hasa wenye majina makubwa kutumia fursa hiyo.

# Usher aonyesha sebule ya jumba lake

Na Mwandishi WETU

MWANAMUZIKI na nguli wa R&B, Usher Raymond ameonyesha muonekano wa kipekee wa sebule ya jumba lake la kifahari lililopo Atlanta, Georgia, Marekani kupitia jarida mashuhuri la Architectural Digest.

Sebule ya jumba hilo, imetawaliwa na sofa ya kipekee ya plasiki yenye mikunjo iliyobuniwa kwa ushirikiano kati ya Usher na mbunifu wa muonekano wa ndani, Nicole Fuller.

Juu ya sofa hiyo kuna mchoro mkubwa wenye rangi za kuvutia uliochorwa na msanii mashuhuri duniani, Damien Hirst.

Katikati ya sofa hizo kuna meza yenye muundo wa kiumbe wa kiasili (sanamu), iliyochongwa na wabunifu maarufu duniani, Campana Brothers.








# Matamasha yatia fora wakuu wa Dabi ya Dar

Na John MARWA

KILA mwenye macho ameona kile ambacho kimeonyeshwa na miamba ya Soka la Tanzania, Simba na Yanga, vikongwe kutoka Kariakoo Dar es Salaam kwenye tamasha lao la 18 la 'Simba Day', na 'Mwannchi Day' 2026, ambapo wamezitambulisha silaha zao za msimu mpya wa Mashindano wa 2026/27.

Walianza Simba katika kilele cha siku yao, ambayo kwao ni utambulisho wa kuanzishwa kwao, Agosti 8, 1936.

Jana ilikuwa ni sherehe za kusherehekea miaka 90 ya historia, vita, changamoto na ukomavu katika maisha ya soka kwa burudani za kila aina na utambulisho wa kikosi chao katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam juzi.

Ukiachilia nyota waliokuwepo msimu uliopita, nyota wapya wazawa ni Kelvin Nashon, Bakari Msimu na Nathaniel Chilambo, huku wageni ni Ibrahim Jabaar, Ibrahim Doumbia, Keletso Makgalwa na wote wameonysha nini wamekuja kukiongeza ndani ya Simba msimu ujao.

Moja ya burudani kubwa la tamasha la Jumamosi ilikuwa ni namna Meneja Habari na Mawasilaino wa Simba, Ahmed Ally alivyoingia katika Uwanja wa Uhuru akiwa na Simba wawili waliofungiwa kwenye kizimba jambo ambalo limeacha alama ya ubunifu katika burudani na ushereheshaji.

Walimalizia wananchi katika kilele cha wiki yao ya Mwananchi ambayo nayo inazidi kukita mizizi ya kuwakutanisha Wananchi wote kwa burudani, utambulisho na mwanzo wa pamoja wa msimu mpya.

Sherehe ya Yanga jana - Jumapili ilikuwa na 'vibe' kubwa na uwanja kuchangamka mno kwa burudani lukuki kuliko ilivyokuwa kwa watani wao, Simba ambapo pia walifungwa na Timu ya Polisi Kenya kwa bao 1-0.

Jana Timu ya Wananchi ilionyesha wachezaji wake wapya na uwanja ulilipuka kwa furaha baada ya kutambulishwa Shalulile.

Wengine walioamsha kelele zaidi ni Farouk Komara, Fred Ngoma, Housseine Zakouani, Albert Kangwada, Ibrahima Toure, huku wazawa wakiwa ni Eric Mwijage, Mohamed Musa, Abdulnasir Muhamed, Hussein Mihambo, na Juma Abushiri.

Sasa kinachosubiriwa na wanachama, mashabiki na wapenzi wa soka ni kuona nini kinavunwa na kila timu na hatimaye kutwaa ubingwa wa ligi ya ndani au nje ya Tanzania.



# ‘Debi’ ya kutoana roho kutikisa







Na John Marwa

BAADA ya kuanika silaha zao za kwenda nazo vitani msimu wa 2026/27, miamba ya soka la Tanzania; Simba na Yanga, zitapepetana katika mchezo wa Ngao ya Jamii, ukiwa ni ufunguzi wa pazia la msimu mpya wa mashindano ya ndani.

Mtanange huo utarindima ndani ya Dimba la New Amani Complex Zanzibar Jumanne - Agosti 12, 2026, kati ya Yanga ambao ni mabingwa wa Ligi Kuu Soka Tanzania Bara (NBC PL), dhidi ya Simba, mabingwa wa Kombe la Shirikisho (CRDB FC).

Hii ni vita, kwani rekodi na heshima vitasakwa mbele ya mashabiki wao. Kinachokwenda kufanyika ni wachezaji wa timu zote kuonyesha kile roho inapenda ama ndo, utanitoa roho itaanza mapema kuchafua shuka la kumbato zito la matarajio ya msimu?

Simba ndio kinara wa mataji ya Ngao, ikiwa imechukua mara 10 kati ya 15 ilizocheza, huku Yanga wakichukua mara 9 kati ya mara 15 ambazo wamecheza.

Ukivitazama vikosi vya timu zote mbili vina mabadiliko ya wachezaji, lakini Yanga ndiyo ina maingizo mapya mengi ya wachezaji ambayo ni zaidi ya 10, wakiwemo nyota sita wa kimataifa wakiongozwa na Peter Shalulile aliyetokea Mamelod Sundowns ya Afrika Kusini.

Kwa upande wa Simba mpaka sasa wamekuwa na maingizo sita huku nyota watatu wakiwa ni wa kigeni wakiogozwa na Ibrahim Doumbia kutoa Mali na watatu wakiwa wazawa.

Kwa upande wa mabenchi ya ufundi, Simba wanaye Steve Barker ambaye amekuwa na timu kwa zaidi ya miezi sita na kucheza dlDebi tatu, akishinda moja na kutoka suluhu moja na sare moja.

Yanga wako na kocha mpya, Manqoba Mngqithi, aliyechukua mikoba ya kudumu ya Pedro Goncalves.

Kufuatia maingizo hayo, kinachosubiriwa ni jibu la nani kucheka baada ya vita yao pale Ungaju viziwani Zanzibar, na nani atawatoa roho mashabiki kuelekea msimu mpya wa mashindano? Jibu ni dakika 90 za jasho na damu kwa kila upande.

*GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa mzunguko – kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.*

TAMPA
TANZANIA MEDIA PRACTITIONERS ASSOCIATION